# *Mara Moja Zaidi*

Ninataka kusema kwamba mimi . . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Ninathamini hilo. Asanteni, sana. Ninataka kusema kwamba hakika ninampenda huyu jamaa, pia. Ndugu Joseph amekuwa rafiki yangu kwa miaka. Ningependa kuwa na nafasi, wakati mwingine, kuwaelezea jinsi tulivyokutana. Bali mimi—mimi ninatumaini tu kwamba Bwana ananipenda kama Joseph anavyonipenda, ndipo nitakuwa sawa basi. Mungu akubariki, Ndugu Joseph. [Ndugu Joseph Boze anasema, "Asante."] Bwana akubariki.

2 Ninaamini tulikuwa tunaenda kuimba huo, "Sasa naamini." Na hebu tumaanishe kutoka mioyoni mwetu, usiku wa leo, "Sasa naamini." Vema.

> Sasa naamini, sasa naamini
> Mambo yote yawezekana, sasa amini;
> Sasa naamini, sasa naamini
> Mambo yote yawezekana, sasa naamini.

3 Hebu tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu, huku tukiendelea kusimama. Na katika wakati huu, hebu tuinamishe mioyo yetu, pia, Kwake. Sasa sijui kama kuna yeyote katika kusanyiko angetaka kukumbukwa katika maombi haya, kwa kuinua tu mkono wako kwa Mungu, ukisema, "Mungu, hii inaonyesha kuwa ningali nina haja, nami ninakutaka Wewe kuikimu." Mungu akujalie haja yako.

4 Baba yetu wa Mbinguni, Yehova Mkuu na Mwenyezi Yule uliyeumba dunia kutokana na Neno Lako, na umetupa fursa ya kupitia hapa na kufanya uamuzi wetu kama tunataka kuishi au kufa. "Chagueni nyinyi siku hii." Na sisi tunachagua kati ya mauti na Uzima. Kwa hiyo ninaomba, Baba, kukiwako na wengine hapa ndani wasiokujua Wewe kama Mwokozi wao wenyewe mpendwa, kwamba usiku huu watakuchagua Wewe, ambao ni Uzima, kujua. Ndipo basi kama kuna wale hapa usiku wa leo ambao ni wagonjwa uletao kifo cha kimwili, kwamba watakuchagua Wewe, usiku wa leo, kama Mponyaji wao, na itamaanisha pia kurejeshwa kimwili tena.

5 Loo, Wewe ni mwema sana kwa wana wa wanadamu, mvumilivu, usiyetaka yeyote aangamie, bali kwamba wote wafikie toba. Wewe hutuma mawingu kwa ajili ya mvua, na kuleta tunda na chakula juu ya nchi, kuwalisha watoto Wako. Na sisi ni wazembe sana, Bwana, na waharibifu sana, kuharibu na kuwa wachoyo. Na, Ee Mungu, tusamehe tu, Bwana. Sisi—sisi tunaomba kwa ajili ya rehema. Tusingetaka haki Yako au hukumu Yako; tunataka rehema Yako, Bwana, kwa hiyo tunaomba kwamba tuweze kuwa washiriki wa rehema Yako.

6 Pia, Baba, si kwamba kusanyiko hili linisikie mimi; bali kwamba Wewe uweze, nikisimama hapa katika mahali hapa ambapo pamewekwa wakfu. Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya ushirika huu mzuri. Pia ninaamini, kwa moyo wangu, kwamba ikiwa Wewe utakuja usiku wa leo, kutakuwa na watu wengi wa New York watakaoenda katika huo Unyakuo mkuu. Tena, Baba, tunaomba ya kwamba tutakuwa nuru, si chini ya pishi, bali chini ya upako wa Roho Mtakatifu ambaye huiwasha taa, ili tuweze kuwa nuru kwa ulimwengu huu unaokufa, wakati giza kuu la ukungu wa kutokuamini linaelea na kuingia kutoka kila upande. Tunajua hivi punde tutamwona Bwana wetu akiupasua ukungu huo, wakati Nuru ikianza kuangaza. Na sisi tunatumaini, Bwana, kwamba Wewe utatufanya tayari. Kama kuna chochote tunachohitaji usiku wa leo, tukirimie, Bwana, kupitia neema Yako. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mtoto Wako. Amina.

7 Mimi si mwenye kuonyesha hisia sana. Bali ningependa kumwambia Mchungaji Vick, maskini mjoli wake pale, na kwaya, kundi la kupendeza la kina mama na wanaume, na wachungaji wote wanaoshirikiana, walei, nyinyi nyote, na wageni, walio wageni malangoni petu. Ninataka kuwashukuru kwa usaidizi wenu juma hili, wa maombi yenu na ushirikiano, kujaribu kuleta Nuru ya Injili katika jiji hili.

8 Na juhudi zetu, Mchungaji Vick pamoja na wachungaji wengine wengi, ni, sisi ni wavuvi katika ziwa hili kuu. Wako samaki hapa ndani ambao ni wa Mungu. Sisi hatujui ni akina nani hao na mahali walipo. Lakini wakati anaposimama kwenye kona moja, mwingine kwenye kona nyingine, wakivua, mimi nimekuja tu kuunganisha jarife langu na yao, pamoja na huduma iliyotolewa, yangu na zao, kujaribu kufikia na kuleta ku—kundi kubwa zaidi kidogo ndani, ili tuweze kuwaleta kwa Mungu, na kusema, "Baba, je! yupo samaki yeyote hapa ndani? Je! kuna mbegu zozote za uzima, zilizokusudiwa kimbele kuwa katika Kitabu cha Uzima, ambazo Mwanakondoo alizifia?" Ikiwa wapo, tunahisi, kwamba wakati Nuru ya Injili itakapowaangazia, wataiona Hiyo upesi, kwa sababu wamekusudiwa hiyo.

9 Sasa tunasikitika kwamba hatukuwa na nafasi ya kuwaweka watu. Kila usiku, karibu, wakati nimekuja, kumekuwa na misongamano mikubwa ya watu kote huku na huko mtaani, wakitembea, wakijaribu kuingia. Huku wengine wakilia; wengine tofauti, mnajua.

10 Lakini ninajua ni kwamba wanayo sheria hapa, sheria ya zimamoto; idadi fulani tu, inakubidi kuacha nafasi fulani katika marefu, na kadhalika. Na hiyo hawawezi kuzuia. Kwa sababu kwamba sisi, kama Wakristo, inatubidi kufanya hivyo. Kwa kuwa Biblia ilisema, Yesu alituambia, "Mpe Kaisari vile vitu ambavyo ni vya Kaisari, na halafu umpe Mungu vitu vile

ambavyo ni vya Mungu." Kwa hiyo tunajaribu kufanya hivyo. Na kama hatutamtii Kaisari, hakuna hakika kwamba tungemtii Mungu. Na mradi tu she—sheria za Kaisari hazihitilafiani na za Mungu, hatuna budi kumtii Mungu kwanza. Na halafu hatari hizi za moto, na kadhalika, vema, wanajua jinsi ya kushughulikia hayo, nao walituambia.

11 Ni—nilikuwa ninaomba rehema kwa ajili ya watu, na kuwaona huku na huko mitaani, na kadhalika, na wagonjwa, na wakijaribu kuingia ndani, na wakiletwa katika teksi kutoka huko mahali pengine katika New York, ama Long Island na Jersey, au mahali mbalimbali, na Manhattan. Vema, mnaona, bali sisi—sisi tunaweza tu kuomba. Ndipo basi wakati nilipogundua kwamba hiyo ni sheria, mbona, alisema, "Kama zimamoto wangeingia na kutukuta tumesongamana namna hiyo, angefunga mkutano wote." Kwa hiyo hiyo ingemkatilia nje kila mtu.

12 Ninataka kueleza shukrani zangu kwa m—m—mmiliki, ama chochote kile kinaweza kuwa, ama kampuni inayomiliki jengo hili, na kwa uongozi kwa kuturuhusu kuwa na jengo hili, na kwa mwangalizi na heshima ya—ya kutupatia haki ya matumizi. Wamekuwa wema sana, sana. Na kama wao . . . Kama wakati huu hawana Uzima wa Milele, ninatumaini kwamba Mungu atawapa Uzima wa Milele.

13 Na sasa hili huenda likasikika kama ta—tamko la kipumbavu, ila nasema hili tu kwa sababu nina juhudi kwa ajili ya Kristo. Ninaomba kwamba ikiwa jengo hili litatumika wakati wowote, baada ya hapa, kwa ajili ya densi ama burudani za kilimwengu, kwamba Roho Mtakatifu atarusha imani kubwa juu ya watu hao mpaka watalia. Ninaomba kwa hilo. Kwa sababu nina hakika kwamba watu hata wanaolimiliki afadhali waone nafsi zikiokolewa kwa Ufalme wa Mungu, kuliko kuwa na huo mwingine ukiendelea.

14 "Na sasa mmekaribishwa kurudi," kwangu mimi kurudi, hilo linajaza tu moyo wangu. Kwa sababu, maskini huduma za kipekee wakati mwingine hazikaribishwi kabisa miongoni mwa ndugu, hasa baadhi yao ambao kwamba katika dhehebu lao fulani kwamba wameinuliwa hadi mahali hata hawawezi kuikubali, unaona, kwa sababu kuna mfumo nyuma yake. Si kwamba wengi wa hao watu wa thamani . . .

15 Nimekutana na makasisi wa Katoliki ambao wamenishika mkono na kuniangalia tu kwenye macho. Na unafikiri sikujua kilichokuwa kikipitia niani mwake? Huo ni utambuzi, unaona, kile unachoona hapa. Alitaka kukumbatia Hilo, bali asingeweza kufanya hilo; unaona, a—angetengwa, unaona. Wahudumu wa Kiprotestanti, vivyo hivyo, ndugu wema, na wao—wao wanataka kufanya hivyo.

16 Kwa njia hiyo, ninapozungumza dhidi ya dhehebu fulani, au mfumo wa kidhehebu, si watu humo ndani. Ni mfumo ndio ninaopinga, unaona, ambao unawatenga, unatuzuia kupokea. Unaona? Wanaweka maazimio yao, wanasema, "Tunaamini *hili,* kituo kikuu!" Kama wangelimaliza kwa koma, "Tunaamini *hili,* pamoja na kiasi kile ambacho Bwana anaweza kutuonyesha kutoka kwenye Neno Lake," ingekuwa sawa. Lakini hawalifanyi namna hiyo. Mnajua hilo. Lisingeweza kuwa dhehebu na lifanye hivyo, unaona. Ingekuwa tu ni uamsho wa Mungu, akitembea kila wakati, unaona. Ndipo ninii . . .

17 Kila mmoja anakuwa mvua ya vuli kwa yule mwingine. Unaona, Luther alikuwa mvua ya vuli kwa Katoliki. Na John Wesley alikuwa ni mvua ya vuli kwa Luther. Pentekoste ilikuwa mvua ya vuli kwa madhehebu. Sasa Wapentekoste wameunda dhehebu, sasa ni nini kinachoenda kufanyika? Unaona? Unaona? Unaona?

18 Lakini kumbukeni, watoto wa Mungu kamwe hawakupigilia mahema yao ya vigingi ama—ama kwa nguvu sana ila ambayo waliweza kuyang'oa. Basi wakati Moto uliposonga, Nguzo ya Moto, walisonga pamoja Nayo. Unaona, walisonga pamoja na Nguzo ya Moto.

19 Bali wakati ukiona Nguzo ya Moto ikifanya jambo fulani, Roho Mtakatifu akifanya jambo fulani, na halafu baada ya mtu huyo aliye na ujumbe kuondoka katika maisha haya, ndipo wanasema wanaunda dhehebu juu ya kazi yake. Ndipo Nguzo ya Moto inasonga moja kwa moja na kutoka na kuwaacha wakiwa wameketi hapo; inasonga tu mbele. Wamepigiliwa vigingi sana mpaka hawawezi kusonga, na, bali humo ndani mna watu wengi wenye moyo safi.

20 Sijui wakati ambapo nimekuwa na uhuru wa kunena tu kilichoko moyoni mwangu kuliko nilio nao papa hapa.

21 Sasa, hapo, wanasema kwamba, "Watu wa New York ni baridi, tofauti, hawana urasmi; kalibu kubwa, ambapo wanachukua kozi moja la wabaya zaidi kutoka kila taifa, na kuwatupa ndani na kusaga, na unapata New York, unaona." Lakini ninataka wewe ujue, humo ndani, baadhi ya watakatifu wa Mungu wako huko ndani pia, unaona. Hiyo ni kweli. Ni kweli. Na kila mahali niendapo, kuzunguka na kuzunguka ulimwengu, ninakuta watakatifu wa Mungu wako katika kila taifa, kila mahali. Na jambo la ajabu ni . . .

22 Huenda nikasema hili kwa baadhi yenu, niingize tu hilo ndani. Kama mmishenari, ni—ninakuta kwamba ninaenda katika taifa ambalo hata halijui ni upi mkono wa kulia au wa kushoto, hawajui maneno yoyote, jinsi ya kuandika chochote, jambo pekee wajualo ni kuua na kula. Lakini hebu watu hao wapokee Roho Mtakatifu, ndipo wanafanya jambo lile lile nyinyi mfanyalo, na kutenda jinsi nyinyi hutenda, bila hata kujua neno

moja kulihusu. Kwa hiyo, mnaona, ni kwa ajili ya jamii zote, watu wote kila mahali, na sisi sote tuna wazuri na wabaya.

23 Basi ninajisikia, usiku wa leo, na kushukuru Baba yetu wa Mbinguni, kwa kuwa ni—ninaamini sehemu hiyo ya ubora wa mazao, ninayo majaliwa ya kuizungumzia, usiku wa leo.

24 Sasa unaweza kuwazia wajibu, kuzungumzia ku—kundi ambalo lingekaa kwenye kila neno usemalo, na ndipo itakubidi kujibu kwa kile ulichowaambia, kwenye Siku ya Hukumu. Kwa sababu, kupitia maskini huduma nyenyekevu, huwapa watu imani kujua kwamba mwanadamu hawezi kufanya mambo hayo. Haina budi kutoka kwa Mungu, hivyo basi wanakaa juu ya kila neno usemalo. Kwa hiyo sijaribu kujenga kitu fulani, kuwazia, au kuandika Maandiko na—na muhtasari kwamba kingekuwa kitu fulani ambacho niliwazia kingewafanya watu kufurahia kabisa. Unaona, ni—ninajaribu kuomba na kuwazia kuhusu kitu ambacho kingekuwa cha kujenga kwenu, ambacho kingewasaidia.

25 Maana, sipo hapa ili tu tupige makofi na kupaza sauti, na kukimbia huku na huko kwenye marefu. Loo, ninaamini katika hilo, hakika, lakini kuna zaidi ya hilo kwake. Haina budi kuwa na msingi kwa ajili ya hili, unaona. Ninaamini kwamba wakati ukiruka, na wakati ukirudi chini, basi ishi juu kadiri ulivyoruka, unaona. Na, usipofanya hivyo, usiruke. Unaona? Kwa hiyo basi daima ruka juu tu kadiri unavyoishi. Na sasa hilo—hilo ndilo tunalopaswa kufanya. Kwa sababu, hata hivyo, unaona, ma—maisha yako hunena kwa sauti kubwa kuliko ushuhuda wako, unajua. Unaona, watu wanajua kile ulicho, kwa jinsi unavyoishi na mambo unayofanya.

26 Na sasa nimeenda kirefu sana usiku. Ninapaswa kuwa nimeondoka hapa, vema, nadhani, kwenye wakati ufaao, katika dakika ishirini zijazo, na hata sijaanza. Na mimi, ni mwenda pole. Ni—ninanii tu . . .

27 Mi—mimi huchelewa daima. Ni—ni—nilichelewa kufika hapa, nilipita kidogo miezi tisa. Na halafu nilikuwa . . . Hiyo ni kweli. Wakati nilipozaliwa, nilikuwa nimepitisha wakati kidogo, mama yangu alisema. Ndipo basi wakati nilipopata, elimu kidogo niliyopata, daima nilikuwa nyuma. Na wakati nilipofunga ndoa, nilimfanya mke wangu kungojea yapata saa tatu hadi nilipomwombea mgonjwa; nilichelewa kwenye arusi yangu. Sasa kama ninaweza tu kuchelewa kwa mazishi yangu, hilo ndilo jambo linalofuata, unaona, hilo ndilo jambo kuu. Sisemi hilo kwa ajili ya . . . Bali hilo ni kweli.

28 Lakini si—sijajaribu kuelimisha watu kuingia katika Hilo. Sijawahi kujaribu kuwazia; kuwacha tu Roho Mtakatifu awe na njia Yake.

29 Ninao wasichana wawili nyumbani. Nilikuwa tu nikizungumza nao, dakika chache zilizopita. Mmoja wao ni

Rebekah, huyo mwingine. . .Huyo ndiye mkubwa. Mdogo, dada anayemfuata, ni Sarah. Na wameachana karibu miaka mitano. Wakati fulani uliopita, nilikuwa kwenye mkutano wa kimishenari, nikarudi nyumbani nimechelewa. Nao ni wasichana wa baba. Na wao hata sasa, Rebekah ni mwanamke kijana, lakini angali ni msichana wa baba. Na mimi ninawapenda watoto wangu. Na ninakumbuka wangeweza kuketi na kungojea. Nisingekuja kwa miezi. Ndipo basi wakati nilipokuja, wangengojea kuniona. Vema, walikuwa wadogo. Imekuwa ni miaka kadhaa iliyopita, yapata miaka kumi iliyopita. Nilikuwa ng'ambo, na nilikuwa ninakuja. Nayo ndege ikachelewa, na kwa hiyo maskini wasichana hao wakashikwa na usingizi na wakaenda kulala. Mtu wa mchanga aliingia machoni mwao, ama alirusha mchanga machoni mwao, hasa. Kwa hiyo basi, vema, mke wangu alingojea.

30 Na hatimaye nikaingia mapema, yapata saa tisa asubuhi. Kwa hiyo basi nilikuwa nimechoka sana na ni mchovu, nisingeweza kulala. Nilijilaza chini kwa yapata saa moja, ndipo nikaamka, nikaenda sebuleni, nikaketi kitini. Na baada ya kitambo, kukapambazuka.

31 Basi muda si muda mwajua, nilisikia kelele huko nyuma chumbani, na ilikuwa hao wasichana wawili walikuwa wameamka. Naye Rebekah alitangulia kuamka, wazo lilimwingia, "Baba yuko nyumbani," na huyu hapa akaja, kutoka kitandani na huyu hapa akaja! Vema, hilo lilimwamsha dada yake mdogo.

32 Na—nadhani watoto wangu ni kama wenu. Wakati mkubwa amevaa kitu karibu kuchakaa, anayefuata hupata cha kupokezana, kwa hiyo Sarah alikuwa amevaa pajama za Becky. Na huo ulikuwa ndio wakati ambapo walikuwa na hizi pajama za mguu-wa-sungura, miguu mikubwa mirefu ndani yake, na bila shaka zilikuwa ndefu sana kwa—kwa Sarah. Na kwa hiyo asingeweza kuchukuliana nazo, miguu yake ilikuwa mifupi sana.

33 Basi kwa hiyo Rebekah alikimbia kuingia na akanirukia gotini mwangu, na kunishika kwa mikono yote miwili na kuanza kunikumbatia. Na, bila shaka, ilinibidi kulia kidogo. Kwa hiyo, na maskini Sarah mdogo alifikiria alikuwa ameachwa nje, Becky alikuwa amemshinda; kwa hiyo alikuwa amesimama mlangoni, na macho yake makubwa meusi yakatazama juu, na machozi mashavuni mwake.

34 Kwa hiyo Rebekah anageuka na akasema, "Sarah, dada yangu!" Alijifanya kitu kama, nafikiri, baadhi ya makanisa yanavyojaribu kufanya, mwajua. Kasema, "Ninataka ujue kwamba nilitangulia kuwa hapa." Ndipo akasema. . .Na alikuwa amenikumbatia kwa mikono yote miwili, ndipo akasema, "Na nina baba wote, wala hakuna kilichokubakia."

Sasa, hilo ndilo wanalojaribu kutuambia, mara nyingi, mwajua. Vema, Becky kwa namna fulani alikuwa na miguu mirefu na kwa hiyo aliweza kufika sakafuni; alikuwa ameimarika vizuri sana, mwajua, kama mengi ya makanisa.

35 Lakini maskini Sarah, aliudhika sana, mpaka nikamwangalia na kumkonyezea jicho langu, mwajua, na kumwashiria namna hiyo. Na kuchomeka goti langu jingine. Hilo ndilo alilokuwa akingojea. Huyu hapa akaja! Ndipo akanirukia mguuni, nao kidogo ulikuwa juu kupita kiasi kwa hiyo miguu yake mifupi, na yeye alikuwa akijifurukuta kana kwamba alikuwa anaenda kuanguka. Vema, nilimshika kwa mikono yote miwili, naye akaweka maskini kichwa chake juu kwenye kifua changu. Na kwa namna fulani alipenda hisia hiyo, nadhani, vivyo hivyo na mimi, kwa hiyo nilikuwa nikimkumbatia.

36 Ndipo akainuka, na akatazama juu kumwangalia Rebekah. Ndipo nikawazia hili lilikuwa jema sana. Akasema, "Rebekah, dada yangu, ninataka kukuambia jambo, pia." Anasema, "Huenda ni kweli kwamba ulitangulia hapa na una baba wote, bali ninataka ujue baba ana mimi wote." Kwa hiyo. . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

37 Mimi si mwanatheolojia. Sikuwa na muda mrefu kutosha kukua katika shule fulani ya theolojia, ila na—natumaini Yeye ana mimi wote, naam, hayo tu, kwa hiyo Yeye anaweza kunitumia.

38 La mwisho, bali si dogo kuliko yote, kwa vyovyote vile. Si—sikuja hapa. . .Nami niliwaomba wasichukue sadaka yoyote, unaona. Si—siji kwa ajili ya hiyo. Sijawahi kuchukua moja, mwenyewe, maishani mwangu. Ninii yangu yote. . .Nimekuwa mhudumu kwa miaka thelathini na mitatu, sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Kuna baadhi zimechukuliwa kwa ajili yangu, na wahudumu. Lakini sijawahi kuchukua moja, maishani mwangu, na ni—ninatumaini haitanibidi kufanya hivyo.

39 Lakini kwamba mmeifanya, itaenda, nitachukua hiyo na kuiweka katika misheni za nje, na kuenda huko, mimi mwenyewe; kuwaleta watu ambao hawana majaliwa mliyo nayo hapa, kuleta Injili ii hii kwa wale ambao hawawezi kumudu kunitumia au kugharamia safari yangu. Hivyo basi. . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Kwamba wao, pia, wasiojaliwa waweze kuwa na majaliwa yaya haya tuliyo nayo hapa. Na hakuna hata peni yake moja itakayotumiwa kwa, mwajua, kunywa pombe, kuvuta sigara, au. . .Itakuwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na mimi ninatumaini kwamba Mungu, katika hilo, atawapa kumbukumbu kubwa. "Kadiri ulivyomtendea mdogo kuliko wote wa hawa, watoto Wangu

wadogo, umenifanyia Mimi." Na ninaomba Bwana awabariki. Na sasa ninaenda kujaribu usiku wa leo . . .

40 Ninataka kuuliza swali moja. Ni wangapi walikuwa katika ule mstari mkubwa wa maombi jana usiku, waliopitia chini ya mikono ya wahudumu hawa, wanaohisi Roho Mtakatifu tayari anashughulikia shida yako? Hebu tuone mkiinua mikono yenu. Loo, hiyo ni ajabu. Hiyo ni nzuri tu, ya kupendeza. Yeye daima hufanya. Yeye hufanya kazi kwa niaba yako.

41 Sasa niliwazia, usiku wa leo, kwa kuwa tumekuwa na ibada nyingi sana za uponyaji . . . Na tumemwona Bwana Yesu katika nguvu Zake kuu, zikimfanya Yeye yule jana, leo, na hata milele. Na tumejifunza kote katika juma, kwamba kumekuwa na ishara nyingi kuu ambazo Yeye ametuonyesha, za Uwepo Wake, papa hapa pamoja nasi sasa, katika umbo la Roho Mtakatifu.

42 Sasa Jumapili ijayo, ninapaswa kuwa kwenye maskani yangu, Jumapili asubuhi na Jumapili usiku, huko—huko Indiana. Ndipo basi juma linalofuata, niko Shreveport, Louisiana, katika mkutano mkubwa. Halafu baada ya hapo, ninaenda Yuma, Arizona. Kisha kurudi Phoenix, kwa ajili ya Wafanyabiashara Wakristo. Halafu kurudi Indiana, kwa ajili ya likizo ya Krismasi.

43 Kisha kurudi Phoenix tena, ikiwa yeyote wenu yuko karibu huko na ana marafiki. Kuanzia tarehe kumi na tisa, wamenipa ule ukumbi mzuri, wa Ramada, unaoketi yapata watu elfu nne, ulioyoyozwa, bure, kabla ya mkutano wa kimataifa wa Wafanyabiashara Wakristo. Ndipo ninazungumza siku mbili usiku kati ya hizo nne, naye Bw. Roberts usiku mmoja na ninafikiri Ndugu Brown usiku mmoja, na ninafikri wangu ndio usiku wa ufunguzi na usiku wa kufunga. Na kisha kutoka hapo, kuendelea na kuendelea.

44 Niombeeni. Na sasa ni—ninahitaji maombi yenu. Kama kuna yeyote anayehitaji maombi, ni mimi, unaona. Na Shetani hakika . . . Mimi ni shabaha kwake, mwajua. Na inanibidi kuhifadhi imani wakati wote, ile ngao, kusonga mbele. Bwana awabariki daima.

45 Na nisipowaona tena mpaka Siku ile, nitakutana nanyi asubuhi, mnaona, kwenye Lango lile. Ndipo basi Kule ndani, ninaweza kusema kama ninavyosema sasa, nitakuwa ningali ninaamini Injili ii hii tukufu, na kuamini kwamba Yesu Kristo hajafa. Bali Yeye yu hai miongoni mwa watu Wake, na Injili Yake ni ile ile. Na mambo ambayo Yeye alifanya, sisi tunapaswa kufanya mpaka Yeye atakapokuja. Pia ninatambua kwamba Mungu atanihukumu kwa mambo hayo ambayo nimehubiri. I—inanibidi kujibu kwa Mungu kwa yale nisemayo.

46 Sasa naomba Bwana awabariki. Basi neno jingine tu la maombi kabla hatujafungua Kitabu.

47 Bwana Yesu, lichukue Neno sasa na uzilishe nafsi zetu zenye njaa. Tunasubiri kwa uvumilivu, Bwana. Tuko chini ya matarajio makubwa. Kama vile kwenye siku ya mwisho ya karamu, jinsi watu walivyoshangilia! Tunawaza kuhusu Simeoni hekaluni, aliyeahidiwa na Roho Mtakatifu kwamba asingeona mauti mpaka alipomwona Kristo wa Bwana. Na hiyo hapo, kwenye ile siku kuu, wakati wanawake walipokuja ili watoto wao watahiriwe, wakatoe zawadi kwa ajili ya utakaso, na ilikuwa ni kwenye wakati huo ambapo Ye—Yesu aliletwa hekaluni. Naye Simeoni, labda nje mahali fulani katika chumba cha pembeni asubuhi hiyo, ofisini, bali Roho Mtakatifu alimtolea ahadi. Na hapa alikuwepo Masihi mikononi mwa mama Yake, Jamaa mdogo huko nje amefungwa katika nguo Yake ya kitoto.

48 Naye Mariamu, wakikaa mbali na yeye, kwa sababu alikuwa na ji—jina baya, ndivyo watu walivyofikiria, "Mtoto huyo alizaliwa nje ya ndoa takatifu." Hakuna mtu aliyetaka uhusiano wowote na mwanamke huyo. Lakini ndani ya moyo wake, alijua Kile alichokuwa ameshikilia mikononi mwake. Basi, Baba, naomba moyo wetu usiku wa leo ubebe tumaini lilo hilo. Haijalishi kile ulimwengu usemacho, tunajua Kile ambacho kimeingia maishani mwetu.

49 Basi kwenye wakati huo, Simeoni, yule ambaye alisema kwamba yeye...Roho Mtakatifu alimwambia kwamba angemwona Masihi. Hata hivyo, akiwa mkongwe, mwenye umri mkubwa, mzee mwenye hekima, mtu mwenye heshima, bali aliamini Neno la Bwana kwake. Roho Mtakatifu akimjia, na, yeye akienda, akiongozwa na Roho Mtakatifu, akiteremka kupitia jengoni, karibu na kundi hili kubwa la kina mama. Kukiwa na watu milioni mbili na nusu wakati huo, usiku kucha huenda kulikuwa na wengi kiasi cha mamia kadhaa ya watoto wachanga waliozaliwa. Nao hao hapo, wamesimama tayari kwa tohara na utakaso.

50 Na jinsi Roho Mtakatifu alivyomwongoza moja kwa moja kwa maskini mtu huyu aliyekataliwa! Akinyosha mikono yake, alimchukua Masihi mikononi mwake, huku machozi yakitiririka kwenye ndevu zake. Alisema, "Bwana, sasa acha mtumishi Wako aondoke kwa amani, kulingana na Neno Lako, kwa kuwa macho yangu yameona wokovu Wako."

51 Akiyumbayumba kupitia jengoni aliingia maskini nabii mke, ambaye Neno la Bwana humjia, na pia akatabiri juu Yake; amepofuka machoni, bali si rohoni. Alijua Huyo alikuwa ndiye Masihi.

52 Bwana Mungu, jalia macho yetu yafumbuke kwa ukweli kwamba Yeye angali ndiye Masihi. Pia jalia tumkumbatie Yeye, usiku wa leo, kwa kuwa tumekiri kwamba sisi ni wasafiri na wageni wa ulimwengu huu. Hapa si nyumbani kwetu. Hii si nchi

yetu. Sisi ni watu wanaotenda tofauti kwa sababu tumezaliwa kutoka Juu.

53 Na sisi tunaoshikilia ahadi hii moyoni mwetu, jalia tuone ahadi ambayo Yesu alilifanyia Kanisa Lake, kwamba tungeona kabla tu ya Kuja Kwake, kama tunavyoona siku za Nuhu zikijirudia, "wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, na utovu wa maadili nchini." Ndipo Yeye akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kwa Mataifa, kabla ya moto kushuka, kwamba Mungu alishuka chini na alidhihirishwa katika mwili, kwa kujua siri za mioyo ya watu." Na Yeye aliahidi jambo lilo hilo kujirudia. Jalia tuwe na majaliwa usiku wa leo, ewe Roho Mtakatifu Mkuu, kwa kuwa kwa unyenyekevu tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

54 [Dada mmoja ananena katika lugha nyingine. Ndugu fulani anatoa tafsiri—Mh.] Amina.

55 Loo, nawazia sasa kuwa makini kuhusu Roho kuwa karibu nasi, Nuru. Jiweke huru kutoka kwenye ganda la saa hii tunayoishi, na wakati, na utambue Roho wa Mungu sasa miongoni mwetu.

56 Hebu tugeukie Kitabu cha Waamuzi, mlango wa 16, kuanzia kifungu cha 23, tunapolisoma Neno.

57 Na wakati mnapofungua, huenda nikasema, wazo langu katika kuchagua mlango huu kusoma alasiri ya leo, katika kufunga mkutano huu, huenda kukawa na kitu kitakacholetwa ambacho kitakuwa cha kulijenga Kanisa. Na daima mimi hungojea kuona kile ambacho Roho Mtakatifu atasema, chumbani, wakati Huyo akinishukia. Huenda nikaandika chini Maandiko mbalimbali na kadhalika, halafu nashangaa kile kitakachokuwa nitakapofika huko. "Yeye atasema nini kuhusu Hili?"

58 Basi sasa sikilizeni kwa makini, jaribuni tu kuwa makini kabisa kwa Hilo kadiri mwezavyo, tunaposoma. Kwa kuwa, hapa ndani, ikiwa ni mapenzi ya Bwana, ninajaribu kuweka mfano, mfano kutoka kwa kimoja hadi kingine. Basi sikilizeni kwa makini sasa, kifungu cha 23, kuanzia.

> Na kisha *wakuu wa Wafilisti wakakusanyika*. . . *pamoja ili kumtolea sadaka Dagoni mungu wao, na kufurahi; maana walisema, Mungu wetu amemtia Samsoni adui wetu mikononi mwetu.*
>
> *Na hao watu walipomwona wakamhimidi mungu wao, maana walisema, Mungu wetu amemtia mikononi mwetu huyu adui wetu,* na aliharibu na kuharibu *nchi yetu na kuwaua watu wengi miongoni mwetu.*
>
> *Ikawa mioyo yao iliposhangilia, wakasema, Mwiteni Samsoni,* ili *atufanyie michezo. Basi wakamwita*

*Samsoni atoke gerezani, akacheza mbele yao; wakamweka katikati ya nguzo mbili.*

*Samsoni akamwambia yule kijana aliyemshika mkono, Niache nizipapase nguzo ambazo nyumba hii inazikalia, nipate kuzitegemea.*

*Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; na wakuu wote wa Wafilisti walikuwamo humo, na juu ya dari palikuwa na watu elfu tatu waume kwa wake waliokuwa wakitazama, wakati Samsoni alipocheza.*

*Samsoni akamwita* Mungu, *akamwita BWANA, akasema, Ee Bwana. . .unikumbuke, nakuomba, ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu, Ee Mungu, ili nipate. . .mara moja kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.*

*Kisha Samsoni akazishika nguzo. . .mbili za katikati ambazo nyumba ile ilikaa juu yake, na ambazo juu yake* yeye. . .*akazitegemea, moja kwa,* na ninii. . . *mkono wake wa kuume, na* kwenye *nyingine. . .wake wa kushoto.*

*Samsoni akasema, Na nife pamoja na hawa Wafilisti. Akainama kwa nguvu zake zote; ile nyumba ikawaangukia hao wakuu, na watu wote waliokuwa ndani yake. Basi wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko wale aliowaua wakati wa uhai wake.*

59 Ni tamasha la huzuni jinsi gani! Hapana shaka ilikuwa ni alasiri yenye joto, jua likiangaza chini kwenye sherehe yake kuu, na Wafilisti elfu tatu walitazama chini kutoka kwenye orofa za juu za uwanja wa michezo, wakati wawili hao walipoingia. Majemadari wa vita wenye heshima kubwa, na wanawake wao waliojipamba kwelikweli, waliinama mbele ili kupata mtazamo mzuri, wakati mvulana huyo alipomwongoza mtu huyu kipofu! Kumbi zilikuwa zimetoa mwangwi alasiri yote kwa shamrashamra za ulevi, wakisherehekea, (hili hapa jambo linaloniudhi mimi) wakisherehekea ushindi wa mungu-samaki wao, Dagoni, dhidi ya mtumishi wa Yehova. Aibu jinsi gani! Jambo la jinsi gani lililokuwa limetendeka! Mtu huyo alikuwa ameshindwa. Sio, Mungu hakuwa ameshindwa.

60 Na kile hapana shaka Yehova alikuwa akiwazia wakati Yeye alipoangalia chini na kuona haya yote yakiendelea! Lundo la wanawake walevi nusu uchi, waliojipamba na kujirembesha, na kutiwa nakshi, waume wao walevi wakinywa pombe na kusherehekea kwa mungu fulani, mungu-samaki, sanamu iliyokuwa imepata ushindi dhidi ya mtumishi wa Yehova.

61 Mvulana huyo alimwongoza mtu huyu kipofu anayejikwaa hadi katikati, ya nguzo—nguzo mahali ziliposimama, mbili ya

hizo, zikishikilia nguzo hizi kubwa zilizoinama, ama ukumbi mkubwa ulioinama chini namna *hii.* Na nguzo mbili kubwa nene, vile ningeweza kuwazia mandhari hiyo; ikiwa na watu, elfu tatu wa majemedari wa vita, na watu mashuhuri, wa—wanajeshi wenye heshima kuliko wote, askari wa vita mashuhuri kuliko wote. Ni kwamba tu watu ma—mashuhuri walialikwa kwenye hii, kwa sababu ilikuwa ni sherehe.

62 Na upande mwingine kutoka kwao kulikuwa na sanamu hii kubwa ya samaki, ikiwa na damu ya mwanadamu chini yake, juu ya madhabahu, kafara kwa huyu mungu-samaki, sanamu ya kikafiri kabisa isiyoweza kuongea, kusikia, wala kupumua. Lakini wao—wao, katika kutokujua kwao, walikuwa wakimwabudu mungu huyu, wakidhania kwamba yeye alikuwa amewapa ushindi, sherehe.

63 Na ndipo akaongozwa kwenye nguzo hizi sakafuni, mahali wote wangeweza kuona, tu—tukio kuu lilikuwa karibu kufanyika. Kulikuwa kumekuwako burudani nyingi, labda kama walivyozoea kuwa nazo, tumbili; na wao walikuwa na wapiganaji na wanyama katika michezo, na wakati wangepigana, na hao wapiganaji na wanyama katika michezo wangesema mhanga (yuko sakafuni) anapaswa kuuawa au sivyo. Na iliwabidi kuona kumwagika kwa damu. Basi ma—matukio yote yalikuwa yamefanyika, na sasa jambo kuu lilifika. Vitangulizi vilikuwa vimemalizika. Nalo tukio kuu lilikuwa ni kumdhihaki Yehova, kumdhihaki Mungu wetu, yote kwa sababu mtumishi Wake alikuwa amempungukia.

64 Unaona, Yeye ni Mungu, hiyo ni kweli, bali sisi ni watumishi Wake na sisi tuna agizo letu la kutekeleza hasa jinsi Yeye alivyosema litekelezwe.

65 Ndipo tunakuta, katika hali yao ya ulevi na kukosa heshima kama waliyokuwa ndani yake, na sasa wote walikuwa wamesimama kwa sababu kulikuwa na kimya kikubwa, labda parapanda ililia. Basi walikuwa wanaenda kuwa na tukio kuu, kwa kile walichokuwa wanasherehekea, kumwingiza shahidi wa Yehova; kumleta hapo nje katikati ya ukumbi, kusudi wote waweze kumdhihaki, na kumfanyia mzaha.

66 Hebu mwangalie, ameaibika, akavunjika, mfano wa ninii—wa kanisa lililoanguka, amevuliwa nguo kiroho, amevunjika kimaadili. Ni mfano wa jinsi gani huo ulio wa hali za leo hii!

67 "Samsoni, huyu alikuwa ni Samsoni, Samsoni mkuu; kwa hiyo huyu alikuwa ni yeye, mtumishi mashuhuri wa Mungu?" Mbona, Wafilisti wengi, ningewazia, hao majemadari wa vita wamesimama hapo, wakitazama hapo; mbona, katika kumbukumbu yenyewe ya jina lake, nchi yote ilitetemeka. Sema tu "Samsoni," hayo ndiyo yote yaliyokupasa kufanya, taja tu jina "Samsoni" na kila mtu alitetemeka jina lake lilipotamkwa, na sasa hebu mwangalie.

68 Unajua, ilikuwa kwamba Jina la "Bwana Yesu" lilikuwa na uchaji mkubwa, watu waliliheshimu Hilo kabisa. Na wale walioliheshimu Hilo wangeweza kufukuza roho ovu, kwa Hilo, na wangeweza kufanya maumbile kutii amri yao, kupitia Jina Lake.

69 Lakini nafikiri kwamba Samsoni hapa, kile ninachotaka kukifananisha nacho, ni ninii ya kisasa ya mahali maalum... au si mahali maalum, bali ha—hali ya kisasa ya kanisa leo hii. Ni mfano mkamilifu. Kanisa limepoteza heshima yake kwa mbali; si kwa sababu kwamba Mungu amelipungukia kanisa, bali kanisa limempungukia Mungu. Haikuwa kwa sababu kwamba Mungu alimpungukia Samsoni, bali Samsoni alikuwa amempungukia Mungu. Ambapo, tunapaswa kuwa tumesimama katika hali kama kanisa lilivyokuwa wakati Anania na Safira walipoletwa mbele ya kanisa. Lakini badala ya hiyo, tumepatana kwa mbali na mambo ya ulimwengu na kuyaingiza ndani, mpaka, leo hii, hilo kuitwa kundi la watakatifu wanaojibingirisha, ama—ama dhehebu lingine tu la kawaida, kanisa fulani tu. Hakuna... Halina, halibebi heshima linalopaswa kuwa nayo.

70 Nadhani, waliposimama pale, wakisimama kwa miguu yao, wakati tukio halisi lilipokuwa linaendelea. Na hebu tujichukulie wenyewe kuwa huko nyuma kwa dakika chache. Basi ningewazia, Wafilisti, wengi wa hao askari mashuhuri wa vita wamesimama hapo, wakiwa na wanawake wao waliojipamba kwa vito, wakiwa wamewakumbatia, wakinywa kwa kumpongeza Dagoni. "Salamu, Dagoni, wewe ni mshindi dhidi ya Yehova! Tumewaonyesha kile tunachoweza kufanya. Tunamwonyesha jamaa huyu, aliyejivunia mengi sana, kwamba hakuna kitu Kwake."

71 Hiyo karibu ndiyo hali ya kanisa leo hii. Sisi ambao tunazo funguo za Ufalme mkononi mwetu, pamoja na kila karama ya kiroho ambayo Mungu alimpa mwanadamu, ikiwa kanisani, kitambo tumepatana na—na kanuni ya imani, na kadhalika, mpaka tumezongomeza nguvu zote za Mungu kutoka kwake, mpaka linakuwa si zaidi ya chumba cha kukutania wanachama.

72 Kama katika tukio la hivi karibuni, wakati Mwislamu alisimama kando ya mwinjilisti wetu mkuu, ndipo yeye akasema, "Nitawaleta watu thelathini ambao ni wagonjwa na wanateseka, na wewe uwaponye kumi na watano wa hao na mimi nitaponya kumi na watano wa hao." Na mimi sisemi hili dhidi ya mwinjilisti huyo, kwa vyovyote vile; lakini mwinjilisti huyo alitoroka na kumwacha huyo mtu peke yake, bila jibu.

73 Jinsi kulivyo ku—ku—kushushwa chini kwa Mungu wetu, kwa kuwa Neno ni Mungu. Na ahadi ya Neno ni ahadi ya Mungu, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

74 Na karibu imefikia usahi mwingine, au sherehe nyingine, wakati miungu ya kikafiri wanapoweza kuzungumzia kanisa,

na kanisa linasimama halijiwezi, limeshindwa, limevuliwa nguo kiroho. Sasa kuna kitu ambacho kimefanya hilo, hicho kimekuwa ni mahangaiko ya ulimwengu kuingia ndani ya kanisa, na lina hayo si zaidi ya chama chochote. Tunaona hilo. Ninaamini . . .

75 Sijui kile ambacho ningefanya katika hali hiyo. Ingenibidi kungojea kuona kile Mungu alichosema. Bali ninaamini ningejisikia kama wale watoto wa Kiebrania, "Mungu wetu anaweza kutukomboa kutoka kwa huu! Lakini, hata hivyo, kamwe hatutasujudia sanamu yako, kama Yeye atatuokoa au sivyo."

76 Bali tumepoteza ujasiri; hilo ndilo Samsoni alilokuwa amefanya, akapoteza nguvu zake. Kanisa limepoteza ushawishi wa ushuhuda wake, kwamba ni Mwi—Mwili wa Kristo, ulio hai, unaotembea. Limekubali mafundisho ya sharti, likayachanganya na imani zao, mpaka Neno halina utangulizi. Kama vile Yesu alivyoliambia lile kanisa lisilojiweza ambalo Yeye alilijia, "Mmezichukua Amri za Mungu, na, kwa mapokeo yenu, mmezitangua Hizo. Mmezitangua Amri za Mungu, kwa mapokeo yenu, kuzieleza Hizo na kuziondolea mbali."

77 Wakati fulani uliopita, katika shule fulani. Kulikuwa na mtu mwema wa New York hapa aliyekuja nyumbani kwangu, naye akaniambia . . . Alikuwa ni ndugu Mbaptisti, na yeye akaniambia, "Ndugu Branham, mimi ni M—Mbaptisti." Ndipo nikamfanya kuingia ndani na kuketi, yeye na ndugu mwingine. Basi tukaongea, kwa, kirefu. Ndipo baada ya kitambo, akasema, "Wakati nilipokuwa mvulana mdogo, niliitwa kwenye huduma." Akasema, "Maskini mama yangu wa thamani alifua nguo kwenye ubao, kunipeleka shuleni." Tena kasema, "Siku ile niliyokuwa ninaenda na kupokea digrii yangu ya Shahada ya kwanza ya Sanaa, shahada yangu ya B.A.," akasema, "Nilidhania hapo hakika Kristo angekuwa katika hiyo, bali," kasema, "Hakuwako." Kasema, "Nilipopata shahada yangu ya uzamifu, basi niliwazia, 'Kristo atakuwa katika hiyo,' bali Yeye hakuweko." Akasema, "Na nilipopata L.L.D. yangu, Daktari wa Fasihi, na kadhalika." Ndipo kasema, "Ninazo shahada za kutosha na shahada za heshima hata ningeweza kukandika ukuta wako kwazo, na yuko wapi Kristo katika hizo zote?" Akasema, "Ningali ninamtafuta Yeye." Kasema, "Ninaenda kukuuliza swali." Anasema, "Je! walimu wamekuwa makosani?"

78 Nikasema, "Ndugu yangu," Mwebrania kwa kuanzia, nikasema, "Sipo mahali ambapo, kama mwe—mwe—mwenye elimu ya daraja la saba, kusema kwamba walimu wamekosea. Ni—ni—nisingesema hivyo. Si—sijisikii kuwa mwenye sifa za kumhukumu yeyote. Bali nitasema hili, kwamba nimempata Yeye, na Yeye hakuwa katika hiyo."

79 Na yeye akasema, “Ninasikia kwamba ulikuwa Mbaptisti.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

80 Ndipo akasema, “Sasa ninasikia kwamba umebadilika kuwa Mpentekoste.”

81 Nikasema, “La. Nimepokea tu Baraka ya kipentekoste, unaona, si dhehebu la Kipentekoste. Baraka ya kipentekoste!”

82 Na yeye akasema, “Vema,” akasema, “Nime—nimekuwa kwenye mikutano yao. Na nimewaona wakipiga teke viti, na kutupa kitabu kupitia dirishani.” Tena kasema, “Usingeweza kuita hiyo tabia ya Roho Mtakatifu mbarikiwa.”

Nikasema, “Bado siwezi kumhukumu Mungu.”

83 Na yeye akasema, “Vema,” akasema, “hivi kile ambacho . . . Ni kitu gani ambacho huwafanya kufanya hivyo?”

84 Nikasema, “Katika kusafiri kwangu, ninakuta matabaka mawili ya watu.” Na nikasema, “Moja ya hayo ni wa kimsingi, kwa nafasi wanajua kupitia mitambo, kwamba wanapaswa kuwa wana na binti ndani ya Mungu.” Tena nikasema, “Jingine ninalokuta ni Wapentekoste, wao pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Lakini nikasema, “Wa kimsingi wanajua nafasi yao mahali walipo, bali hawana imani yoyote katika Neno. Nao Wapentekoste wana imani nyingi, ila hawajijui ni akina nani.” Ndipo nikasema, “Ni kama mtu aliyekuwa na pesa kwenye benki, bali asingeweza kuandika hundi; na mwingine angeweza kuandika hundi, bali hakuwa na pesa kwenye benki. Laiti ungaliweza tu kuwaweka pamoja!”

Akasema, “Vema, ni kitu gani kinachowafanya kutenda namna hiyo?”

85 Nikasema, “Ni kutoa mvuke.” Nikasema, “Sasa, sidhani hiyo ingebidi kuhitajika,” nikasema, “bali wao inawabidi kuwa na mahali pa kupumulia mahali fulani.” Na nikasema, “Sasa iwapo wangeweza tu kuchukua mvuke huo wote na wangeweza kujua jinsi ya kuuelekeza kimsingi, katika Neno, utawala mkuu wa Mungu ungeanza kufanya kazi.”

86 Hapo ndipo Shetani alipoingilia, kufanya yote kuwa mitambo bila ya nguvu tendaji. Kwingine, yote nguvu tendaji wala hakuna mitambo. Unaona, inatubidi kuziweka pamoja. Tuna nguvu za Roho Mtakatifu, bali inatubidi kurudi na Neno ili kulisha mashine hii. Hatuwezi kuilisha kwa kanuni ya imani. Haitawasha moto; huziba mabomba ya hewa, na haitawasha moto. Ilitengenezwa kwa ajili ya Neno la Mungu. “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno,” sio tu sehemu Yake, “kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

87 Kwa hiyo hapa tunasimama, Kanisa lililoagizwa kwa agizo la mwisho, jambo la mwisho ambalo Yesu aliliambia Kanisa Lake, agizo la mwisho lililotolewa, “Enendeni ulimwenguni kote, mkafanye wanafunzi kwa mataifa yote. Yeye aaminiye na

kubatizwa ataokoka; yeye asiyeamini atahukumiwa. Na . . .” *Na* ni kiunganishi, kuunganisha sentensi yako pamoja. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, hakitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

88 Kwa hiyo ni kwa nini itubidi kusimama mbele za mungu fulani wa kikafiri na kukubali kushindwa? Tunasimama tena kama Samsoni, tumevuliwa nguo kiroho, tumevunjika kimaadili, makanisa yetu. Ni kitu gani kimetendeka, wao—wao walikuwa ni wanaume na wanawake wa heshima, na leo hii wewe—wewe . . . ni jambo la kuogofya. Sasa hebu tuangalie dakika chache tu kwenye baadhi ya mawazo yaliyopita juu ya hili. Kwa hiyo pale akasimama Samsoni, na, samahani, huyu hapa tena leo hii, tena amevuliwa nguo kimaadili, kiroho. Na vile vile ni mfano wa taifa lililoanguka. Ila tunazungumza kuhusu Kanisa, kwa sababu Samsoni alikuwa ni mtumishi wa Mungu, alidhaniwa kuwa, nalo Kanisa linadhaniwa kuwa ni mtumishi wa Mungu duniani.

89 Askari wengi wakuu wa vita wakisimama pale, kutoa ulevi kwa kitambo, wakati pombe ikiisha kwenye ninii yao . . . labda silaha zao na deraya za kifua, huku mikono yao imewakumbatia malkia wao warembo, waliojipamba, walipoangalia nje kule, na wengi wao wakitazama tamasha hii. Mvulana mdogo akimshika hili bonge la mtu, huku hakuna macho kwenye mashimo yake; yalikuwa yamechomwa na kutolewa.

90 Hilo ndilo adui hufanya. Kitu cha kwanza, wakati anapokushika, yeye hufanya kama alivyomfanyia Samsoni. Yeye hufunga macho yako usione Nuru ya Injili. Sasa hawezi kuona. Macho yake yamekwisha. Muda mrefu kanisa limepoteza macho yake ya kiroho, kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kila ahadi ni kweli.

91 Na wanaposimama hapo sasa, hakuna macho, tamasha ya aibu, aibu kusimama chini ya mungu-samaki, mateka wa taifa lile lile ambalo Mungu alimwinua kuangamiza.

92 Sasa ninaenda kuja nyumbani kwa dakika moja. Na hawa hapa watu wetu Wapentekoste ambao, miaka hamsini iliyopita, waliondoka kwenye matope hayo ya madhehebu, Mungu alituita tutoke na tuwe watu waliotengwa. Basi tunasimama, leo hii, madazani tu ya madhehebu, mbalimbali, na Pentekoste yote yakipigana moja na lingine. Kitu chenyewe hasa ambacho Mungu alituita tutoke na kukishinda, kimetushinda. Kama mmoja akienda kwenye dhehebu hili, ana mkutano, wengine hawataki kushirikiana. Sasa hivi tu na halafu unaweza kupata moja. Hiyo ni kweli. Na dhehebu daima limekuwa ni laana machoni pa Mungu. Kamwe haikuwa; Mungu kamwe hakufanya hivyo. Huo kamwe haukuwa mpango Wake.

93 Mungu hawezi kubadilisha mpango Wake. Mungu hushughulika na watu binafsi. Kulikuwa na mamilioni katika siku za Nuhu, bali Nuhu alikuwa ndiye aliyepakwa mafuta. Kulikuwa na mamilioni katika siku za Eliya, kamwe si Elisha na Eliya kwa wakati mmoja. Kote chini, kila kizazi! Kulikuwa na milioni mbili na nusu huko Misri; Musa aliteremka chini. Unaona? Kulikuwa na mamilioni katika siku za Yesu. Hata wakati Yohana nabii mashuhuri aliposimama, wakati alipomwona Huyu Mwenye nguvu aliye mkuu akija, alisema, "Sina budi kupungua sasa, kazi yangu imekwisha; na Yeye ataongezeka, Mungu." Aliwaelekeza kwa Mwana-kondoo.

94 Lakini, unaona, hiyo iliendelea kwa miaka mia tatu, hadi Baraza la Nikea, ndipo basi ilibidi tuwe na dhehebu. Halafu kuanzia hapo, hilo lilianguka. Basi kila wakati ambapo ujumbe hutokea, nao wanauundia dhehebu, hufa kiroho na kamwe halirudi tena. Kwa hiyo ni kitu kilicholaaniwa, kwa Kanisa la Mungu, kwa mwanadamu kuweka mkono wake juu ya uamsho wa Roho. Daima.

95 Ndipo wanawapeleka huko nje na kupata wahudumu wa seminari, nao wanachangamana na ulimwengu, na kadhalika. Muda si muda wajua, walikuwa na wanawake wakitenda kama walimwengu, wanaume. Kitu cha kwanza unajua, siasa na maaskofu, na wao wanataka jani katika kofia yao, na wao wanakata na kusukuma, na kuzozana na kupigana, mpaka Roho wa Mungu anahuzunika kabisa na kuondoka.

96 Baadhi yao wanakumbuka kumwona Samsoni wakati upako ulipokuwa juu yake. Amesimama uwanjani, na Wafilisti elfu moja wamelala karibu na yeye, bila chochote mkononi mwake ila maskini mfupa mkavu wa taya la nyumbu mwepesi wa kuvunjika, ambao alikuwa amepiga kupenya helmeti zenye unene wa inchi moja, akiwaangusha Wafilisti upande mmoja na mwingine, wakati Roho wa Bwana alipokuwa juu yake. Na wengi wao walikuwa wamekimbilia kwenye mwamba. Na yeye akisimama pale, akisema, "Kama unataka baadhi yake, jitokeze!" Baadhi yao wanakumbuka kuona hilo.

97 Baadhi yao huenda walinong'onezana, na kusema, "Je! unakumbuka huko Gaza usiku ule, wakati ilipotangazwa kote kwamba adui yetu alikuwako mjini? Nasi tukachukua jeshi, tukafunga malango. Nayo malango, yakiwa na uzito wa labda tani sita au saba, malango hayo makubwa ya shaba, ambapo magari manne au matano yote ya farasi yangeweza kupitia, jeshi likiingia mjini. Na sisi tukachukua jeshi, pamoja na mikuki yetu na panga, na tukasimama na kusema, 'sasa tumempata.' Na wakati tulipoamka!" Alitembea tu moja kwa moja katikati yao, akiwasukuma kulia na kushoto; akachukua lango na kung'oa moja, na kung'oa hilo jingine, na kuliweka mabegani mwake, akapanda juu ya mlima na kuketi chini. Hapo ni wakati Roho wa Bwana alipokuwa juu yake. Siku moja . . .

98 Baadhi yao huenda walikumbuka wakati walipoona simba akimngurumia, ambaye angemwua katika sekunde moja.

99 Kama yeyote anajua kile, jinsi simba anavyoweza kukuua haraka. Na kwa kishindo kimoja na mngurumo, punde wanaua ko—kongoni mwenye uzito wa tani mbili ama kifaru; kwa moja tu la hayo makono yenye makucha, kuvunja shingo yake namna *hiyo*, ama kumwuma namna *hiyo*, na yeye amekwisha. Hata hapigi teke, huwaua mara moja kabisa.

100 Na hapa mtu huyu akitembea hapo, ndipo simba akanguruma, na yeye alikuwa bila msaada wowote, si hata mfupa wa taya la nyumbu mkononi mwake. Bali Biblia ilisema, "Roho wa Bwana alikuja juu yake," ndipo akamnyakua simba na kumrarua vipande.

101 Lakini sasa amesimama, hajiwezi, amevuliwa nguvu zote. Ni kitu kile kile sasa, kanisa linasimama jinsi hiyo. Ambapo, wakati mmoja kanisa lilikuwa likitoa pepo. Kanisa lilikuwa likifufua wafu. Kanisa lilikuwa likifanya mambo ambayo Yesu alifanya. Dhambi isingeweza kukaa miongoni mwao, Roho Mtakatifu aliingia na kuihukumu. Iwapo mtu alifanya jambo kisiri, na alikuwa mshiriki wa kundi hili la Kikristo; punde tu alipoingia, Roho Mtakatifu alifichua dhambi yake. Yeye ama alitubu au aliangamia. Lakini, unaona, hatunaye tena.

102 Wala hawatampokea tena. Na wakati akija, wanajaribu kumwita "roho mwovu," ili waweze kupokea hukumu zaidi kiasi hicho. Kitu fulani hakina budi kuwahukumu.

103 Tazama, amevuliwa nguvu, ni kitu gani hapana shaka kilipitia niani mwa mtu huyo? Wakati mmoja askari wa vita namna hiyo, na sasa mvulana mdogo hana budi kumwongoza huku na huku. Kwa nini? Yeye ni kipofu. Hawezi kuona. Hana chochote cha kuona kwacho.

104 Mungu, turehemu! Kanisa limejiundia dhehebu sana na limeenda mbali sana, mpaka ibilisi ameng'oa macho yake ya kuona, macho ya kiroho kwamba *Hili* ni Neno la Mungu. Si kanuni ya imani; Hilo ni Neno! Na Mungu anawajibika ku—kuleta kila kitu ambacho Yeye aliahidi katika Biblia hii. Wanasema, "Sisi, tunaamini . . . " Huna imani yoyote inayokuja, ikiwa ni kinyume na Hili. Nia ya Kristo ndani yako, unaamini mambo ambayo Kristo aliandika, maana *Hili* ni Kristo, Neno. Lakini angalia hali, angalia mfano, wakati tukiona hilo.

105 Ni kitu gani ambacho hapana shaka kilipitia niani mwake? Hebu tuone kilichopitia niani mwake.

106 Tunaona kilichopitia niani mwa majemadari wa vita, ya hofu waliyokuwa nayo wakati mmoja kwa jina lake tu. Waliogopa kufanya lolote. Wanataja tu Samsoni, hayo ndiyo yote, kila mtu alitoweka. Bali sasa huyo hapo, amesimama, mateka chini ya Dagoni, mungu-samaki. Myahudi aliyedharau sanamu, alikuwa anasimama mateka chini ya moja (kwa nini?) kwa

sababu alikuwa amempungukia Mungu. Samsoni akisimama pale, hapana shaka . . . Hebu—hebu—hebu tuchunguze nia yake kwa yapata dakika tatu au nne. Hapana shaka aliwazia ushindi wote aliokuwa nao. Huyo hapo amesimama, kile alichokuwa ametenda. Jinsi Bwana alikuwa amembariki, na jinsi ambavyo wakati mmoja alikuwa ni mtu mashuhuri mradi tu alikuwa katika Ufalme wa Mungu, akishikilia ahadi ya Mungu!

107 Unaona, alikuwa ameshindwa, na kuondolea mbali ahadi. Hilo ndilo jambo lile lile kanisa limefanya, kuondolea mbali ahadi. "Loo, vema, hilo ni, tutaandika maskini katekismo yetu wenyewe, *hii*, unaona." *Hili* Ndilo, Neno!

108 Sasa, angalia, alikuwa amewazia kuhusu ushindi wake wote. Ndipo basi hapana shaka hili lilimpitikia niani mwake, na jinsi ambavyo alikuwa amewaaibisha watu wa Mungu.

109 Inapaswa kuwa aibu, kwa mhudumu ambaye ataketi na kusoma Biblia hii kisha ajitokeze mbele za watu wake, ulimwengu umejaa kina Lutu. Biblia ilisema kwamba "dhambi za Sodoma ziliitesa nafsi yake yenye haki," bali hakuwa na ujasiri kusimama na kukemea dhambi hiyo. Na kuna watu wengi leo hii . . .

110 Nami ninasema hili kwa kicho, ila tu kwa—kwa upendo, bali ili tu kusema Kweli. Huenda tusikutane tena.

111 Wapo watu wengi ambao husoma Biblia ii hii ambayo sisi husoma; anaketi katika ofisi yake, akitayarisha ujumbe wake, na kukumbana na Kweli hizi za Mungu, na inambidi kuzikwepa. Angeogopa kuhubiri dhidi ya wanawake kukata nywele zao. Dhehebu lake lingemtupa nje. Kuhusu wao kuvalia nguo za kizinifu na kufanya uzinzi wa kiroho. Na kuhusu wanaume ambao—ambao hunywa kileo kwenye Krismasi, na—na kutoka nje na kuwa na burudani ndogo safi ya Kimarekani, anatoa mizaha michafu, angali anashikilia ofisi kama shemasi. Wanajua mambo hayo ni makosa, bali wako kama ilivyokuwa katika siku za Lutu. Tumerudi kwenye mahali hapo pa dhambi tena. Unaona?

112 Loo, jinsi Samsoni hapana shaka alikumbushwa, na Roho Mtakatifu, jinsi ambavyo alikuwa amewaaibisha watu wa Mungu, na alikuwa amempungukia Mungu mwenyewe. Sasa yeye ni mfungwa wa kitu kile kile ambacho Mungu alimwinua na kumpa nguvu kuangamiza.

113 Na kwa upendo na kwa . . . Mimi ni mshiriki, mimi niko katika Hili pamoja na nyinyi; si mshiriki wa dhe—dhehebu, Mungu azuie. Bali mimi ni mshiriki, kwa neema, katika Mwili wa Kristo. Mimi ni ndugu yenu. Sina malengo ya kichoyo, lengo langu kufanikisha kitu chochote mimi binafsi. Mimi nina juhudi kwa ajili ya Bwana Mungu pekee, na ninasema hili kwa—kwa moyo wangu wote. Kitu chenyewe hasa mlichoitwa kutoka kwacho, mmerudi ndani yake tena. Na kama Biblia ilivyosema,

"Kama nguruwe anavyoenda kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kurudi kwenye matapishi yake!" Na kama matapishi yalimchefua mbwa, hapo mwanzo, si yatamchefua zaidi mara ya pili? Na kama madhehebu na kanuni za imani ambazo zilikuwa zimewafunga watu sana, na Mungu akawaita mtoke ili mwe watu huru, na nyinyi mkageuka moja kwa moja mkarudi na kufanya jambo lile lile, itakuwa, ni dhambi kubwa zaidi.

114 Sasa walikuwa naye akiwafanyia vitimbi kuwatumbuiza. Na hivyo tu ndivyo karibu limefikia, badala ya Roho Mtakatifu.

115 Kwamba wakati mtu anapoinuka na kuwa na kiburi, Roho Mtakatifu anawajibika kwa Mungu, kukifunga kitu hicho. Nimewaona wakiwabeba kutoka kwenye mkutano, wamepooza, vipofu, bubu, na hata wanakufa moja kwa moja kwenye mikutano, na kuanguka na kufa huku wakijaribu kukemea Hilo. Mungu Mbinguni anajua hiyo ni kweli. Wengi wenu hapa mmekuwa katika mikutano mingine na kushuhudia jambo lilo hilo.

116 Kunapaswa kuwa na Nguvu takatifu zikizunguka, na ndani ya kanisa, ambazo zitafanya pepo kutoroka. Badala ya hizo, limekuwa kitu cha kuchekwa. Ni kitu gani? Mitambo badala ya nguvu tendaji.

Sasa anafanya vitimbi.

117 Ni nini kilichosababisha hayo, ni nini kilichosababisha kuanguka kwa Samsoni? Alimruhusu mwanamke kumshawishi kuacha ahadi ya Mungu. Hiyo ni hakika. Sote tunajua hiyo. Alikuwa na vishungi saba. Na yeye alizaliwa, ukoo wake wa kuzaliwa, alikuwa awe ni Mnadhiri, jamaa wa kipekee, kwa Bwana. Lakini, unaona, alimwacha mwanamke huyu kumshawishi mpaka akanyolea mbali upekee wake.

118 Na hilo ndilo jambo lile lile ambalo limefanyikia kanisa. Mmezaliwa watu wa kipekee, taifa takatifu, ukuhani wa kifalme. Lakini kulifanyika nini? Mmeuachia ulimwengu kunyoa na kuondoa upekee wenu mpaka mmekuwa mmoja wao. Iliwabidi kuwa na dhehebu kama tu walivyokuwa nalo. Iliwabidi kung'aa kuliko Baptisti au Wamethodisti, moja. Na sasa Waassemblies wanajaribu kung'aa kuliko wa Umoja, na wa Umoja kung'aa kuliko wa Assemblies, church of God linashinda hili, na loo, jamani, kuendelea na kuendelea, madhehebu thelathini au arobaini mbalimbali. Unaona, kama mbwa akirudi kwenye matapishi yake, kitu kile kile.

119 Angalia, kitu hicho hicho kimefanywa kama kilivyokuwa wakati ule, kumrusu Yezebeli, "mama wa makahaba," Ufunuo 17. Kumbukeni, yeye aliitwa kahaba, huyo ni mwa— mwanamke mzinzi. Na mwanamke daima huwakilisha... Kanisa linawakilishwa na mwanamke. Kwa sababu, Kristo, yule ambaye Yeye anamjia ni Bibi-arusi. Na yeye alikuwa "mama wa makahaba." Mwanamke mzinzi ni kitu gani? Sasa, isingeweza

kuwa mwanaume, kwa sababu walikuwa "makahaba," unaona. Ni mwanamke ambaye angeishi bila uaminifu kwa mume wake. Na yeye anadai kwamba ndiye mama wa makanisa yote, na ndivyo alivyo.

120 Na ni kitu gani kilichomfanya kahaba? Ni kwa sababu alifanya uasherati wa kiroho. Alichukua kanuni za imani badala ya Neno la Mume wake. Badala ya kuwa mwenzi mwaminifu wa amri, kwa mume wake, yeye alichukua kitabu kingine, cha kanuni za imani. Na yeye alikuwa ni kitu gani? Mama wa makahaba waliofanya jambo lile lile. Sasa huhitaji maelezo zaidi kwa hilo, unaona. Unaona mahali lilipo. Ilikuwa ni kitu gani? Dhehebu, kuliondokea Neno.

121 Angalia sasa kile Delila alichomfanyia Samsoni wakati aliposhikilia kumchumbia. "Loo, wewe ni mtu mashuhuri. Wewe ni mwenye nguvu. Lakini, usinidanganye, niambie zilipo nguvu zako." Na yeye alimpenda, na akamfanyia mapenzi mpaka hatimaye alisalimu amri. Basi walifanya nini? Kitu cha kwanza mwanamke huyo alichofanya, alifanya siri yake kuondolewa kwake.

122 Vema, hicho ndicho kitu kile kile kilichofanyika (na nyinyi wasomaji na wanafunzi wa Biblia) kwenye Baraza la Nikea. Njia ya kale ya pentekoste ilitaka kudumu na Neno. Na wao wakachukua mawazo fulani ya kipagani kupitia Konstantino na hao, na kuleta . . . Kama Ahabu alivyomwoa Yezebeli na kuingiza uabudu sanamu katika Israeli, vivyo hivyo kanisa liliolewa katika Urumi na kuingiza uabudu sanamu, kurudi moja kwa moja kanisani tena.

123 Sasa mna kundi dogo la makahaba, juu ya misingi ile ile, basi tazameni kinachoendelea sasa. Mama anafanya ubembe, na tena anaenda kunyoa haki zenu zote na kuziondolea kutoka kwenu. Mungu saidia kwamba kamwe tusiachilie Hilo; ni Neno hili au mauti! Baraza la Makanisa, wakijiweka pamoja na kuungana katika ushirika kuzunguka Rumi, kile hasa Biblia ilichosema ingefanya.

124 1933, Roho Mtakatifu alikuja asubuhi moja na kuniambia mambo saba ambayo yangetukia kabla ya taifa hili kuangamizwa. Moja ya hayo ni hilo. Liko kwenye gazeti la kale kule kanisani, wengi wamelitazama. Jinsi ambavyo tungeenda vitani na Hitler na wangeninii . . . Jinsi Ujerumani ungeimarisha na kujenga Ngome ya Maginot, au Ngome ya Siegfried, ninaamini ilikuwa, miaka kumi na moja kabla haijawaziwa kamwe. Na jinsi ambavyo motokaa zingeendelea kuchukua umbo la mayai. Na jinsi ambavyo wangewaruhusu wanawake kupiga kura, na, katika kufanya hivyo, wangemchagua Rais asiyefaa. Na katika hili kungekuwa na mwanamke atakayeinuka ambaye ataongoza Marekani; si hasa mwanamke, bali kanisa.

Ndipo nikamwona akiwa hana kitu ila majivu. Linaenda kutokea.

125 Matano kati ya mambo hayo yametimizwa kikamilifu hasa. Jinsi ambavyo Mussolini angeinuka na kuenda Ethiopia, na kuanguka katika hatua zake; na yeye angegeuzwa kwa watu, katika aibu, akiwa na mwanamke. Miaka mingi, mingi sana kabla halijatendeka kikamilifu kabisa. Na kamwe halijashindwa, wala halitashindwa, kwa sababu ni BWANA ASEMA HIVI. Na si tofauti na hii Biblia. Sharti iwe.

126 Sasa yeye anafanya mapenzi kwa binti zake, akiwashawishi kuwarudisha moja kwa moja nyumbani tena. Bila ya ufahamu wa kiroho, wamevuliwa, ni oasisi kwake. Wanasema, "Loo, jinsi kilivyo kitu kikuu." Loo, jamani! Na watu wa Kipentekoste wameketi katika baraza huko Rumi, na kutuma nyaraka kote, kwamba, "Ulikuwa ndio wakati wa kiroho kuliko zote walizowahi kuona." Mtu aliyezaliwa mara ya pili anawezaje kukatilia mbali siri yake, kukatilia mbali Neno, na waishi kwa kanuni ya imani? Hicho hasa ndicho Delila amefanya leo hii, kukatilia mbali Neno halafu unaishi kwa kanuni ya imani.

127 Sasa tazama kushindwa, leo hii, kutoka kwa kile kingekuwa. Wahudumu, badala ya wahudumu walioitwa na Mungu kwa ajili ya kundi letu la Kipentekoste, karibu inakubidi kuwa—kuwa na shahada ya udaktari kabla hujaweza kuingia mimbarani. Unaona? Hiyo ni kweli. Kitu cha kwanza, inakubidi kuwa na kadi ya ushirika. Na ikiwa wewe . . . Na sasa katika madhehebu yetu makubwa ya Pentekoste, kabla hawajamtuma mmishenari, inawabidi kumpeleka mbele za mtaalamu wa magonjwa ya akili, kuona kama anaweza kustahimili jaribio la akili. Vema, hiyo si Presbiteria, kwamba hiyo ni Pentekoste. Unaona? Sasa hiyo ni kweli. Sasa, nisingesema hilo isipokuwa ningeweza kulitetea. Unaona, unaona? Kweli. Niambieni kama hiyo ndiyo sifa ya mhudumu.

128 Biblia ilisema, kamwe hawakuenda mbele ya mtaalamu yeyote wa magonjwa ya akili, "Bali walingojea katika mji wa Yerusalemu, mpaka walipojazwa na Nguvu kutoka Juu." Baadhi yao wasingeweza kuandika jina lao. Siku chache baadaye, mmoja alipitia lango liitwalo Zuri, na yeye hakuwa amewahi kuwa mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya kiakili. Kamwe hakuwa na kadi yake ya ushirika, bali alisema, "Kile nilicho nacho!" Sijawahi kuona kadi ya ushirika ikileta hayo bado.

129 Sisi ni kitu gani? Tumevuliwa nguo, tukaaibishwa katika Uwepo wa Roho Mtakatifu. Hutimiza hasa kile nabii alichosema katika Timotheo wa Pili 3, "Litakuwa kaidi, lenye kiburi, wenye kupenda anasa kuliko kumpenda Mungu." Ilikuwa ni kosa kwa wanawake wetu Wapentekoste kuenda kuogelea wamevaa nguo ya kuogelea, na kuogelea mchanganyiko. Si kosa tena, unaona. La, la, kama tu ulimwengu, vile vile tu.

Mambo haya yote, unaona, kilimwengu. Kila kitu kilichoko ulimwenguni, walikiingiza tu ndani, na wahudumu wameinuka na kuwaruhusu wake zao kufanya hivyo. Nao wamefanya aina hii yote ya upuuzi, na kizazi hiki kinaendelea kukua, na ndipo kinachofuata kinaingia. Ninii tu . . . Loo, jamani!

130 Samsoni alisimama, akiwazia ushindi wake mkuu. Hebu tutazame nyuma na kuona ushindi mkuu wa mwanzoni wa Pentekoste. Haikubidi kutazama mbali miaka elfu mbili iliyopita, tazama tu nyuma miaka hamsini iliyopita. Pia, kumbuka, kanisa la Katoliki ya Rumi kwanza lilikuwa ni kanisa la kipentekoste. Na wao wanasema ya kwamba, "Kanisa lilizaliwa, na kwamba kanisa la Kirumi lilizaliwa Nikea, Rumi." Ninataka Andiko kwa hilo. Kanisa la kwanza kamwe halikuanza Nikea, Rumi. Kanisa la kwanza lilianzia huko Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste. Loo, mhanga wa makosa yote! Loo!

131 Ndipo wakati yeye alipotambua mahali alipokuwa amesimama, wakati alipotambua kile ambacho kingetokea.

132 Kama nilivyosema, huenda nisiwaone tena. Sijui. Huu huenda ukawa ndio Ujumbe wangu wa mwisho kwenu. Huenda mimi, kama nikininii . . . Bwana akiruhusu, na nirudi mwaka ujao, sisi sote hatutakuwa hapa. Ha-ha. Baadhi yetu watakuwa wameondoka. Na kila mara, lazima ninene kana kwamba ilikuwa ni mara yetu ya mwisho; maana ndivyo ilivyo, baadhi yetu. Huenda ikawa ni mara yangu ya mwisho.

133 Ni hali ya jinsi gani, kosa! Na iwapo tungesimama tu kama Samsoni alivyofanya, na kuwazia kwa muda mfupi tu kile tunachopaswa kuwa, kwa Biblia ya Mungu. Si kitu fulani kikubwa, si kuenda, kushikamana na kina Jones; bali kundi la watu wanyenyekevu, wenye kicho, waliojazwa na Roho. Si linalong'aa; linalomeka. Hollywood hung'aa, Injili humeka. Unaona, tunataka kitu kinachong'aa, makanisa makubwa kuliko yote tuliyowahi kuwa nayo. Tungekuwa bora zaidi, tulisimama huko chini uchochoroni, katika kibanda, na kuwa na Roho wa Mungu akirudi juu yetu tena. Hiyo ni kweli. Angalia.

134 Basi wakati aliposimama pale na kutambua, na nywele zake zilikuwa zimeanza kukua tena; ila asingeweza kufanya yaliyotakiwa, kwa sababu hakuwa na macho yoyote. Ndipo akalia, "Bwana, lipiza kisasi macho yangu. Wamening'oa macho."

135 Wao, leo hii huenda nikasema, ni kanuni za imani! "Walinipeleka kwenye seminari. Na wito uliokuwa moyoni mwangu, wa Mungu aliye hai, walitoboa huo kabisa na kuuondoa kwangu, wakisema, 'Mambo hayo yalikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine.'"

136 "Lipiza kisasi macho yangu!" Samsoni alikuwa akiwaza nini? "Kulikuwa na uwezekano, labda. Yehova amejawa upendo. Yeye, huenda inawezekana kwamba Yeye atanisikia."

137 Loo, laiti ningaliweza kumfanya Samsoni kutambua hilo usiku wa leo, kuna uwezekano! Yeye amejawa upendo, akisamehe uovu wa watu Wake, kutoka kizazi hadi kizazi, akiwarehemu maelfu wanaompenda Yeye na kutii Amri Zake.

138 "Kuna uwezekano," Samsoni aliwazia, "laiti ningalipata tu kulipiza kisasi kwa ajili ya macho yangu. Siwezi kuona mambo hayo tena. Hayatokei."

139 Hatuwezi kumwona Roho Mtakatifu mkuu, katika madhehebu yetu makubwa, akitembea kama Yeye alivyofanya mwanzoni. Limekwisha. Unaona, hayupo hapo. Ni kipofu, wala halijui. Yesu alisema ungekuwa hivyo, Wakati huu wa Kanisa la Laodikia. "'Tajiri,' asema, 'Mimi ni tajiri, na nimejitajirisha, na sina haja ya kitu.' Nawe hujui kwamba wewe ni uchi, kipofu, mwenye mashaka, mnyonge, nawe hujui." Unaona, hujui!

140 Vema, tulikuwa na usemi, "1944, milioni moja zaidi," dhehebu fulani. Na kupitia huduma ya mtu mashuhuri, wamekuwa na milioni moja zaidi ya kitu gani? Wenye kujiunga. Hiyo ni kweli.

141 Alijua kulikuwa na uwezekano, lakini jambo ni kwamba, leo hii, watu hawaonekani kupata ufahamu kwamba kuna uwezekano. Wameridhika kuendelea moja kwa moja mwelekeo wa kale wanaoenenda. Unaona, usifanye hivyo. Mwamini Mungu! Msadiki Yeye.

142 Sasa wanasema, loo, wao, "Sisi tutakaa imara." Hiyo ni kweli. "Tunapiga makofi yetu, na—na kila kitu, na kupaza sauti." Lakini nyinyi mlikuwa tu maneno matupu bila matendo. Unaona?

143 Mnawezaje kupiga makofi yenu na kupaza sauti, na kukana Neno kuwa Kweli? Mnawezaje kupiga makofi na kupaza sauti, naye Roho Mtakatifu atatembea miongoni mwenu, halafu nyinyi mnasema, "Loo, ni kuwasiliana kimawazo. Ni—ni kitu fulani, hakifai tu kabisa"? Unaona? Unaona?

144 Tunayo mikutano mikubwa, mng'ao, mapambo ya kilimwengu, mikutano mikubwa, tunapata nini? Wafuasi zaidi. Kanisa la Kipentekoste, miaka mitatu iliyopita, limeingiza wafuasi wengi ndani yake kuliko mengine yote yalivyofanya pamoja. Hiyo ilikuwa katika *Mgeni Wetu Wa Jumapili*, jarida la Katoliki. *Mgeni Wa Jumapili* lilisema walikuwa na waongofu milioni moja kwa Katoliki mwaka huo, na kusema, "Wapentekoste walikuwa na milioni moja laki tano." Naam. Naam, bwana.

145 Kila namna ya usomi, watu waliofunzwa kuzungumza, katika shule, na kutoa hotuba zao, wenye elimu, watu wa maonyesho ya Hollywood, samahani tamshi hilo, wakihubiria kundi la wanaojiita wajukuu wa Pentekoste!

146 Mungu hana wajukuu. Wanaingia. Maskini baba na mama wa kipentekoste, chini ya tukio, walikuingiza ndani; na wewe unakuja tu kanisani na kuketi hapo, na moja kwa moja ulikuwa mpentekoste? Yeye hana wajukuu. Yeye anao wana na binti pekee. Hakuna wajukuu. Inakubidi kulipa gharama ile ile na kupata Roho Mtakatifu yule yule waliyempata. Inakubidi kuwa mwana na binti, si mjukuu wa kiume na mjukuu wa kike. Yeye si babu mkongwe aliyepungua akili na nguvu, dhaifu, na huachilia wajukuu wake kupita na chochote, kutakia heri maskini mioyo yao. Yeye ni Mungu, Yule wa Milele! Hiyo ni kweli, wana na binti!

147 Tungali tuna mwili mkubwa kama Samsoni alivyokuwa nao. Alisimama hapo na nguvu zake zote. Alisimama hapo mkubwa tu kama alivyowahi kuwa. Na sisi tunasimama wakubwa kuliko tulivyokuwa, lakini tumevuliwa nguvu. Samsoni angali alikuwa na misuli yenye nguvu, alikuwa angali na kila kiungo cha mwili alichokuwa nacho, ila Roho wa Bwana hakuja juu yake tena. Tumesimama, milioni wenye nguvu, wenye nguvu kuliko tulivyokuwa, lakini yuko wapi Bwana. Kama Malaika alivyosema huko nyuma katika siku za Gideoni, alisema, "Ikiwa wapi na ikiwa kungali na Mungu, wapi miujiza Yake? Wapi mambo anayopaswa kufanya? Ni wapi ambapo Yeye anajithibitisha Mwenyewe, kwamba Yeye yu hai, na ni yule yule jana, leo, na hata milele?" Hilo ndilo tunalopata.

148 Angalia, Samsoni aliomba vizuri. Samsoni aliomba, "Bwana, jalia nife na adui," wakati alipotambua kilichokuwa kinaendelea karibu naye. Macho yake yalikuwa yameondolewa. Nguvu zake zilikuwa zimekwisha. Ushirika wake ulikuwa umetoweka. Bali kulikuwa na uwezekano kwamba mkutano wa maombi ungeweza kuutia moto tena. Unaona? Ndipo akaomba vizuri, "Jalia nife pamoja na adui."

149 Lazima ufe na adui wako. Hiyo ni kweli. Huna budi kumfia adui huyo aliyekuingiza katika hali hii. Hiyo ni kweli.

150 Samsoni alikuwa tayari kulipa gharama ili kufanya nguvu za Mungu kurudi juu yake tena. Aliona kile alichoinuliwa kufanya. Si kuwa mtu wa maonyesho; bali kuwa mtumishi, kujiweka mwenyewe ili kwamba nguvu za Mungu ziweze kutembea kupitia yeye.

151 Tumesimama, mamilioni wenye nguvu kuliko tulivyokuwa, bali nguvu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kusudi.

152 Yesu hata alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo nafsi nane ziliokolewa na maji, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwa Mwana wa Adamu." Hawa wote mnaoona wakitembea mtaani ni chakula cha mizinga. Ni chakula cha atomiki, imewekwa tu hapo kwa ajili ya hukumu. Unyakuo unakuja, kutakuwa na wachache mno. "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, na, bali ni wachache ndio watakaoiona; kwa

kuwa njia ni pana ielekeayo katika uharibifu, na ni wengi wanaoenda huko. Si wote wanaoniambia Mimi, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia, bali yule afanyaye mapenzi ya Baba Yangu." Huyo ndiye ambaye huingia, unaona; si kusema "Bwana," na maombi yao mazuri, na—na miamsho, na kadhalika.

153 Loo, ninamsikia mtu fulani akisema, "Sasa ngoja dakika moja, Ndugu Branham, tunayo miamsho." Naam. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Tunayo miamsho, na ni kitu gani tulicho nacho? Ni uamsho wa kimadhehebu, kuona kama tunaweza kuingiza wengine zaidi kanisani.

154 Na sisi tunao uamsho mwingine mashuhuri, pia, tunaingiza makanisa yote ndani ya moja, Baraza la Makanisa. Naam, tukienda mbali zaidi na zaidi na Neno la Mungu, wakati wote. Kuunganika! "Wawili wanawezaje kutembea pamoja isipokuwa wamepatana?" Tunaendaje kutembea na watu ambao wanakana kufufuka kwenyewe kwa Kristo? Tunawezaje kutembea na watu ambao walisema, "Siku za miujiza zimepita"?

155 Nyinyi ni watu waliotengwa, na Roho Mtakatifu. Unaona? Ulimwengu unataka, leo hii, ninii—ninii—ninii. . . Kile ulimwengu unachotaka leo hii ni wachanganyaji. Wanataka mtu fulani ambaye anaweza kutembea kote na—na kushirikiana na ulimwengu na kushirikiana na watu, na kupata washiriki wengi, na kuwa na shirika la kijamii. Bali wakati Roho Mtakatifu aliposema, "Nitengeni Mimi Paulo!" Mungu ni mtenganishaji, si mchanganyaji. Mtenganishaji!

156 Alijua kwamba nguvu zake zilizorudi nyuma, ingawa hapo zilisimama zote, mamlaka makuu aliyowahi kuwa, alisimama pale, lakini nguvu zake zilizorudi nyuma hazingeweza kukabiliana na changamoto ya wakati huo.

157 Nalo kanisa linajua hilo, pia. Mwinjilisti alijua hilo wakati yule Mwislamu alipomsai. Nguvu zako za kiakili hazikabiliani na changamoto ya wakati, maana ibilisi ameachiliwa miongoni mwetu, akiwa na nguvu ambazo hakuna kitu kiwezacho—kiwezacho kuthubutu kukabiliana nazo ila Roho wa Mungu Mwenyezi, wakati Neno hili likifanyika mwili. Na inaenda kuwa mbaya zaidi na zaidi, mbaya zaidi daima.

158 Alijua kwamba alipungukiwa. Asingeweza kufanya hilo. Pia alijua kile ambacho kingetendeka kama Mungu alijibu maombi yake.

159 Sijui ikiwa tuko tayari hivyo usiku wa leo? Sijui kama ulimwengu wa Kipentekoste uko tayari, usiku wa leo, kufanya maagano yayo hayo na Mungu? "Bwana Mungu, kama ikivunja dhehebu langu vipandevipande, kama wakinitenga kutoka kwenye baraza! Sijali kama wakichukua kadi yangu ya ushirika, na inibidi kulala njaa, na kunywa maji ya tawi na kula mkate mkavu, badala ya kuendesha huku na huku katika motokaa kubwa na mshahara mkubwa! Sijali ni nini

gharama. Mfumo huo ulinipeleka mbali na Wewe. Nitwae tena, Bwana. Nitaliamini Neno Lako. Lipiza kisasi macho yangu yaliyong'olewa. Jalia nife na huo. Amina. Jalia nife kwa nafsi yangu. Sijali kile wanachosema juu yangu. Huenda nikawa askofu, huenda nikawa *hili, lile,* au *linginelo*, sijali kile wanachosema. Rudisha nguvu za Roho Mtakatifu katika maisha yangu. Nimepofushwa muda mrefu vya kutosha."

160 Loo, kanisa, je! mko tayari kwa ajili ya hilo? "Jalia nife na wengine wote. Jalia jina langu, kama kasisi, daktari, ama chochote kile, liangamie. Ee Mungu, nipe tu tena, tuma tu juu yangu tena, hizo Nguvu tukufu zilizoshuka kwenye Siku ya Pentekoste; zinazoweza kukabiliana na changamoto ya wakati huu, usoni pa ukomunisti au chochote kingine kinachoinuka. Jalia nife, Bwana, pamoja nao." Kuna uwezekano, unajua.

161 Unajua nini? Juu ya maungamo kama hayo, Wafilisti, walikuwa wamelewa kupindukia hata wasingeweza kutambua kile alichokuwa anafanya. Mara moja, alipoona kulikuwa na uwezekano, aligeuza kichwa chake juu kuelekea angani, na machozi yakitoka kwenye mashimo yaliyopofuka. Alianza kuchezesha midomo yake; machozi yakianguka kutoka machoni mwake. Hawakuwa wakimtambua. Walikuwa wanashughulika sana kumdhihaki. Alitaka Neno la Mungu, Mungu wa kweli aliye hai kuja jukwaani mara moja zaidi. Alikuwa amemwaibisha Yeye. Alijua alimwaibisha Yeye. Bali alitaka kumwona Mungu aliye hai, akiishi hapa, kuthibitishia hao wa namna ya Yezebeli kwamba Yeye angali alikuwa ni Mungu.

162 Loo, kama ikitoa ugumu kutoka kwako, kama ikikufanya kutojiadhibisha kama bingwa fulani wa sinema, kama ikikubidi kuacha nywele zako zikue, na kuvalia gauni la mtindo wa kale, "Sijali inagharimu nini. Nitafuata njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Bwana, jalia tuione tena, jalia tuone Uwepo wa Mungu ukitembea mbele za huyu Yezebeli!"

163 Alijua kilichotendeka kama Mungu alijibu maombi yake, bali alikuwa tayari na katika juhudi kubwa.

164 Hilo ndilo litupasalo kufanya. Kuwa tayari, fanya maamuzi. Funga macho yako, acha shauku zako. . . Usibadilishe Neno la Mungu kwako; jibadilishe mwenyewe kwa Neno Lake. "Si mapenzi yangu; Yako yafanyike, Bwana. Si kile ninachowazia juu yake; ni kile Wewe ulisema juu yake." Hiyo ni kweli.

Alilia nini? "Bwana!"

165 Kasema, "Mvulana mdogo, weka mmoja wa mikono yangu juu ya nguzo hii. Inawezekana." Loo, jamani! "Niongoze kwenye nguzo inayoshikilia hili, kwa sababu ninataka kupumzisha mikono yangu. Nimechoka. Nimechekwa, muda mrefu vya kutosha." Loo jamani!

166 "Ninajua, Bwana, kile kinachoenda kugharimu, lakini labda Wewe utafanya. Kuna uwezekano. Wewe umejawa rehema.

Nimekupungukia Wewe, Bwana." Hicho kinapaswa kuwa ndicho kilio cha kanisa, usiku wa leo.

"Mvulana mdogo, waweza kuweka mkono wangu juu ya nguzo moja?" "Naam."

"Na mkono wangu juu ya nguzo hiyo nyingine?"

"Naam."

"Je! mikono yangu imewekwa vizuri."

"Naam, iko sawa."

167 Ndipo akaanza kuomba. Na akasema, "Bwana, lipiza kisasi macho yangu." Kwa maneno mengine, "Nimefanya kosa. Lakini mara moja tu zaidi, Bwana, mara moja zaidi!"

168 Loo, laiti hilo lingekuwa ndilo kusudi la huduma ya Pentekoste usiku wa leo! "Niko tayari kusahau kuhusu kama niko hivi, ama umoja, uwili, utatu. Niko tayari kusahau kuhusu mambo haya yote ya ulimwenguni na kila kitu. Mara moja tu zaidi, Bwana! Mara moja zaidi niondoe kwenye kanuni hii ya imani na kitu hiki ambacho nimefungwa ndani yake! Mara moja zaidi! Mara moja zaidi jalia nione kuonekana kwa Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Kanisa lingelia hicho, ingawa wamepofushwa kutokana na mambo haya, wamepofushwa kutoka kwa ndugu yao na wazo lake. Lichukue tu wazo la Mungu na haitakubidi kubishana kuhusu Hilo. "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!"

169 Ndipo pale ulisimama ule mwili mkubwa, bila nguvu na bila uwezo wa kujisaidia. Mara ghafla, alianza kuhisi kitu fulani kikitendeka. Kila mshipa wa mwili wake ulianza kujaa na Nguvu za Mungu.

170 Loo, laiti kanisa lingaliweza tu kufikia hizo tena, na kote kuanzia kwa mhubiri hadi kwa shemasi, hadi kwa walei, kila mshipa na kila kiungo cha mwili kingejazwa na Nguvu za Mungu!

171 Misuli hiyo mikubwa yenye nguvu ilinyooka, ndipo akaitiisha pamoja. "Jalia nife pamoja nao, Bwana! Jalia nife pamoja nao! Uliniinua kuliangamiza. Sasa nimejijenga mwenyewe kulizunguka; jalia nijiangamize mwenyewe pamoja nalo, umaarufu wangu na chochote kilicho. Jalia niliangamize, lakini ninataka kuona Nguvu za Mungu tena."

172 Daima, wakati Nguvu za Mungu zikija, kuta ulizojenga kukuzunguka, huporomoka. Kuta zako za kimadhehebu zitaporomoka, na Mungu atajulikana tena. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

173 Kila mfupa wake ukijaa na Roho Mtakatifu, kila musuli ulijazwa, kila sehemu ya mwili wake ulikuwa umejazwa kabisa

na Roho Mtakatifu. Huo ulikuwa ushindi mkubwa kuliko wote wa Samsoni.

174 Loo, Kanisa la Mungu aliye hai! Ninaenda kuacha muhtasari wangu uliobaki, kusema jambo hili moja. Kwa nini hatufanyi hivyo? Je! mko tayari, Assemblies of God? Mko tayari, nyinyi, Kanisa la Umoja? Mko tayari, Umoja, Utatu, chochote mlicho? Mko tayari, kanisa la Mungu? Mko tayari, enyi madhehebu mengine yote, kusahau upuuzi huu na jambo ambalo mmefanya? Tazameni mahali mmefikisha watu, usiku wa leo, na namna ya hali waliyomo.

175 Ee Mungu, jalia tuvunjilie mbali kuta hizo. "Mara moja zaidi, Bwana!" Sijali, tuko kwenye mwisho wa wakati, jamani. Hatuna mengi yaliyosalia. Heri tuwe tukipiga makelele sasa hivi, tukilia. "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Mara hii tu zaidi, kwenye mwisho wa ulimwengu, jalia nguvu Zako zijaze kila mshipa wangu. Nitajiondoa kutoka kwa mambo haya yote. Kadi za ushirika, na maaskofu, na madhehebu, na kila kitu, havimaanishi chochote kwangu. Ninakutaka Wewe, Bwana, zaidi ya chochote."

176 Hebu tuwazie hilo, huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi. Nimesukumwa kufanya hili. "Mara moja zaidi, Bwana!" Kila mtu, kwa uaminifu, kwa uchaji, kwa kicho tu uwezavyo kuwa. Kuwa tu na imani, na chini ndani ya moyo wako useme, "Mara moja zaidi, Bwana!"

177 Bwana Yesu, Bwana Mkuu wa Uzima, Mchungaji wa kondoo, njoo, Bwana. Watu hawa wana njaa. Wanaona kiu. Bwana, miaka nimetaka kuona hili likitendeka, labda litatendeka. Mara moja tu zaidi, Bwana, mwendo mmoja zaidi mkubwa wa Roho! Mara moja tena, Bwana, na Kanisa huenda likapokea imani ya unyakuo kuingia ndani. Tujalie, Bwana. Fanya ijulikane kwamba Wewe uko pamoja nasi, na sisi tutakusifu Wewe kwa ajili yake. Katika Jina la Yesu tunaomba hayo. Amina.

178 Ninajua si maneno mengi, ninajua si maombi marefu, bali Yeye anajua kusudi langu. Nilimaanisha hilo. Je! Yesu anaweza kuishi miongoni mwetu usiku wa leo? Je! Yesu anaweza kutujia sisi na kuonyesha kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, jinsi ambavyo tumefundishwa? Je! yupo mgonjwa au anayeteseka, au aliyevunjika moyo, hapa ndani, ambapo—ambapo mnajua hakuna kadi za maombi zilizotolewa (tulizichukua zote jana usiku), bali unaamini Mungu, unaweza kuinua mkono wako na useme, "Nina hitaji, Ndugu Branham. Ninamwomba Mungu kwamba Yeye atanizungumzia"? Inueni mikono yenu, popote. Ni kila mahali.

179 Sasa hii hapa (kitu gani?) neema ya Mungu kushuhudia kile nilichosema ni Kweli, unaona. Unaona, mwanadamu anaweza kusema chochote; isipokuwa Mungu athibitishe hilo, basi ni uwongo. Sasa wewe amini.

180 Nami ninakutaka uniamini mimi kama mtumishi Wake. Ninataka umwambie Mungu...Unaona, wakati Yeye alipokutana na mimi, Yeye alisema, "Kama utawafanya watu wakuamini wewe, na halafu uwe mwaminifu."

181 Na sasa iwapo Yesu alisimama hapa, usiku wa leo, na kama ulikuwa mgonjwa au mhitaji, chochote kile, Yeye asingeweza kukuponya; Yeye tayari amekuponya. Lakini Yesu na Neno ni kitu kile kile. Yeye ni Neno. Na Yeye alisema, "Mtu anapaswa kuishi kwa Neno hili," si kwa kanuni ya imani. Kwa Neno! "Na Yeye aniaminiye Mimi," si anayejifanya kuamini, bali aaminiye, "kazi nizifanyazo mimi atazifanya pia."

182 Angewezaje Yeye kutambua kilichokuwa niani mwao? Alifanyaje hilo? Na wao walidhania Yeye alikuwa akisoma mawazo yao; ndipo Yeye akawaambia Yeye angewasamehe kwa hilo, "Bali Roho Mtakatifu ajapo kufanya hilo, kunena dhidi ya Huyo hakungesamehewa kamwe." Sasa tumepitia hilo, moja kwa moja kupitia kwenye Biblia, na kuona kwamba Mungu, kama Yeye alijitambulisha Mwenyewe wakati ule kama Masihi, kwa kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii na Neno. Kwa sababu, Biblia ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," Waebrania 4, "na Mtambuzi wa mawazo yaliyoko moyoni." Hiyo ndiyo sababu wasingeweza kuficha chochote kutoka Kwake. Na kadhalika, hivyo, hivyo ndivyo walivyojua.

183 Hivyo ndivyo yule mwanamke kisimani alivyojua Yeye alikuwa Masihi. Akasema, "Bwana, naona kuwa Wewe ni nabii. Sisi tunajua, wakati akija Masihi, Yeye atatuambia mambo hayo. Hayo ndiyo atakayofanya."

Akasema, "Mimi Ndiye."

184 Akaingia mbio na kuwaambia watu, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia yale—yale niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Nao wakaamini hilo.

185 Lakini kwa njia fulani sisi hatuamini, inaonekana kana kwamba ulimwengu hautaki kuamini hilo. Lakini, Mungu aliye mwingi wa rehema, ni uwezekano kwamba Yeye huenda akafanya hilo tena. Inambidi Yeye kujitambulisha Mwenyewe namna hiyo, Masihi. Hawezi kulifanya kwa Wasamaria na Wayahudi, na halafu awaache Mataifa nje. Haina budi kufanywa, kwa hiyo wewe omba na uguse upindo wa vazi Lake.

186 Na kwa makasisi. "Yeye ndiye Kuhani Mkuu sasa awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli, Waebrania 3.

187 "Sasa Yeye ndiye Kuhani Mkuu," sisi sote tunaamini hilo, "awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele." Basi Uhai Wake, matendo Yake, kila kitu Chake ni kile kile. "Kitambo kidogo,

na ulimwengu," kosmos, utaratibu, "hautaniona Mimi tena," kamwe hawataona hilo.

188 Kumbukeni Malaika aliyeshuka chini, katika umbo la mwanadamu, alizungumza na—na Ibrahimu, aliyeitwa atoke, Kanisa teule. Yeye kamwe hakuenda Sodoma na kufanya huko chini kama jamaa wale wengine walivyoenda huko chini na kuhubiri, kama Billy Graham na hao leo hii, pamoja na hiyo G-r-a-h-a-m tena, kama A-b-r-a-h-a-m. Unaona? Kila mmoja, tazama, walikuwa na mjumbe wao. Wanaye leo hii, kitu kile kile kinakuja. Nenda hapa juu kwenye Kanisa lililoitwa litoke, ambao hawakuwa huko Babeli, na huko ndiko kitu hicho cha ajabu kilifanywa; wakati Yeye alipomwambia Sara, wakati alipokuwa ndani ya hema nyuma Yake, kilichokuwa shida.

189 Alicheka. Ndipo Yeye akasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake, kwamba, 'Mambo haya hayawezekani'?" Ndipo Ibrahimu akamwita, na yeye akajaribu kukana hilo. Na Yeye akasema . . .

190 Tazama, hii hapa neema. Huu hapa—huu hapa uwezekano. Mungu angalimwua, papo hapo, lakini Yeye asingalifanya hivyo; yeye ni sehemu ya Ibrahimu. Kwa kutokuamini kwetu Yeye angetuua, lakini Yeye hawezi; sisi ni sehemu ya Kristo. Neema inatushikilia. Mnaona? Lakini Yeye angali inabidi adumishe Neno Lake.

Sasa nyinyi ombeni.

191 Simwoni mtu ambaye kwa kweli ninamjua, ndani ya jengo. Ila Ndugu Pat Tyler anayeketi hapa mwisho, ninamjua. Lakini kadiri . . . Na ninafikiri Ndugu Bill Dauch anayeketi papa hapa, na mke wake. Nje ya hao, hao ndio watu pekee ambao ninawajua, Ndugu Joseph. Na kama Roho Mtakatifu angewazungumzia, nitawaambieni tu ni nini kuhusu hayo, na ndipo niache hayo na kuwaambia baada ya ibada.

192 Lakini mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! "Kazi nizifanyazo Mimi, nyinyi pia mtazifanya." Sasa nyinyi amininі, na mwone kama Nuru ile ile mnayoiona kila mara . . .

193 Vema, tulipomalizana na Nyakati za Kanisa, huko chini katika maskani, yapata watu wengi hivi. Wapo watu walioketi papa hapa sasa walikuwepo. Nguzo ile ile ya Moto ilikuja moja kwa moja upande wa ukuta, na kuchora hizo Nyakati za Kanisa jinsi nilivyokuwa nazo ubaoni. Je! hiyo ni kweli? Wengi wenu mlikuwako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nao watu wakizimia, na kila kitu kingine. Nikasema, "Ile pale sasa, iwapo kuna swali."

194 Wanayo picha Yake, hapa katika Washington, DC, imepewa hakinakili kama "Kiumbe cha pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha." George J. Lacy, mkuu wa F.B.I. hati ya alama za vidole, alichunguza Hiyo, wakati Nuru hiyo ilipokuwa pale. Na yeye akasema, "Ndugu, Bw. Branham,

nilisema ilikuwa ni saikolojia. Nimehudhuria mikutano yako; lakini jicho la kimitambo la kamera hii haiwezi kupiga picha saikolojia, unaona." Kasema, "Nuru iligonga lenzi."

195 Vema, kama huyo ni Kristo aliyemwangusha Paulo chini, na akamwita Yeye, "Bwana," unaona, "Wewe unataka nifanye nini?" Uhai uliokuwa ndani Yake utazalishwa tena ndani yetu, basi. Unaona, Yeye yupo hapa pamoja na Kanisa lililoitwa litoke.

196 Na ninaomba itimie, mara moja zaidi, Bwana, kwamba watu hawa waweze kuona kwamba Wewe ungali hai. Na Wewe hujafa, na wala Wewe hujawaacha watu Wako. Wapo hapa, bali, Bwana, macho yao yameng'olewa na madhehebu, Yezebeli Delila, ambaye aliwaondoa kwenye Neno la kweli, hadi kwenye kanuni ya imani. Naomba kuta ziporomoke, Baba. Jalia hilo. Mara moja zaidi, Bwana! Kama nilivyosema, wapo wengi hapa ambao labda sitawaona tena. Lakini mara moja zaidi, Bwana, jalia Yesu aonekane miongoni mwetu, katika umbo la Roho Mtakatifu; ili Yeye aweze kuzalisha Uhai ndani yetu, ambao Yeye alikuwa wakati ule, kutimiza Neno Lake.

197 "Yeye ndiye Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Jalia wagonjwa na wanaoteseka wamguse huyu Mwalimu. Wewe ni Yule yule, Bwana, ambaye aliweza kumwambia Simoni Petro, wakati alipokuja miongoni mwao, "Mbona, jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Wewe ni Yule yule, Baba. Hushindwi. Yule yule, maskini mwanamke aliyegusa vazi Lake, Kristo yule yule anaishi usiku wa leo. Jalia iwe mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Kwa ajili ya Yesu naomba hilo. Amina.

198 Sasa hakuna mtu anayesogea. Kwa kicho, hebu tuwe na uaminifu na kicho kabisa. Hatuyaendei mambo haya ovyoovyo.

199 Ni ahadi ya Mungu. Roho wa Kiungu wa Mungu aliye hai aliahidi hilo katika Neno Lake, nalo Neno hilo ni Uzima na Roho. Yesu alisema lilikuwa. Na Yeye na Neno ni sawa, na mtu huishi kwa hilo Neno. Neno hilo huishi ndani ya mwanadamu.

200 Sasa, kama karama. Sasa ninaenda kuwaambia siri, ninapoondoka. Mmekuwa wema na wenye fadhili. Sijawahi hasa kutamka hili, nijuavyo, hadharani, hapo kabla. "Ndugu Branham, ni nini karama hiyo?" Ni karama ya kujua jinsi ya kumwondoa William Branham njiani, ili Yesu Kristo aweze kuishi kupitia chombo. Kujiondoa tu mwenyewe njiani!

201 Sikujui wewe. Sijui chochote kulihusu, lakini Yeye anajua. Yeye Ndiye.

202 Sasa kuwa na imani, na uamini. Useme, "Bwana, mtu huyo hanijui. Na hata hivyo Wewe ulisema, 'kitambo kidogo, ulimwengu,' Babeli, au Sodoma, hautakuona Wewe. 'Bali nyinyi mtaniona Mimi. Mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, kote kote hadi mwisho wa ulimwengu.'"

203 Haujafika mwisho bado. "Nyinyi mtaniona Mimi. Nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Mtaona Uhai Wake ukizalishwa tena ndani ya waaminio.

204 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti wangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kusudi kazi za Mungu ziweze kujulikana tena, kama Yeye akiona inafaa kufanya hivyo.

205 Si zaidi ya nilivyolisema neno hilo, nilitazama hapa kwenye kona, na hapa. . . Hamwezi kuona ile Nuru inaning'inia moja kwa moja pale, kaharabu, ikisogea huku? Ama ni, je! niko katika kiwango kingine, na ninawaza tu, roho yangu?

206 Yupo maskini mwanamke aliyeketi pale. Yuko taabuni. Anasumbuliwa na shi—shida ya tumbo. Na yeye amefanyiwa upasuaji, kwa ajili ya kansa, na kansa hiyo ilikuwa kwenye titi. Waliondoa kansa hiyo, maskini mama. Naam. [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hiyo ni kweli.

207 Kwa hiyo sasa utajua. Sikujui, lakini je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Nitalisema wazi, usiku wa leo; ninaondoka. [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.] Je! unaniamini? ["Amina."] Je! unaamini kwamba tumeahidiwa kwamba katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4, kwamba "atageuza mioyo ya watoto imwelekee Baba"? ["Amina."]

208 Mbona, Bibi Taylor, hilo ndilo jina lako. Unaweza kwenda nyumbani, na Yesu Kristo akufanye mzima. [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

209 Unafikiria nini? Umefanyiwa upasuaji, pia. Unaamini? Kama unaamini, kwa moyo wako wote! Upasuaji wako pia ulikuwa wa kansa, uvimbe, katika matumbo, eneo la matumbo. Bali sasa unasumbuka na matatizo. Kama utaamini, Bibi Shukwit, kwa moyo wako wote, kwamba Yesu Kristo atakufanya mzima, unaweza kupata kile ulichoomba.

Je! unaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

210 Hapa, mama hapa nyuma, yeye ni mama mweusi. Anasumbuliwa na shida fulani na macho yake, pia na viungo vyake, miguu yake. Jina lake ni Bibi Washington. Simama, ukipenda. Umeponywa.

211 Aligusa kitu gani? Uliza kile alichogusa. Unyenyekevu wa huyo mama mweusi . . .

212 Licha ya hayo, Hiyo ilimshukia mama mwingine mweusi aliyeketi moja kwa moja hapa nje kwenye mwisho. Anaugua ugonjwa wa moyo. Jina lake ni Bibi Harris. Je! unaamini, Bibi Harris? Shida yako ya moyo imekuacha.

213 Aligusa nini? Kamwe hakunigusa mimi. Yuko yadi ishirini kutoka kwangu. Alimgusa Kuhani Mkuu.

214 Hapa, hapa yupo mwanamke mwingine, ninageuza kichwa changu, anayeketi moja kwa moja hapa. Yeye anaugua ugonjwa wa moyo, pia. Bibi Carter, simama, Yesu Kristo anakufanya mzima.

215 Huko nyuma, mwanamke aliye na tumbo lenye vidonda. Jina lake ni Bibi P-a-o-l-i. Bibi Paoli, simama, Yesu Kristo alikuponya. Vema. Haya basi.

216 "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Je! mnamwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

217 Hebu tusimame. Hebu tuungame dhambi zetu, na kuomba, "Mara moja zaidi, Bwana, jalia Roho Mtakatifu ashuke juu yetu!" Tuinue mikono yetu.

218 Bwana Mungu, tunasimama tumeaibika; ulimwengu unatudhihaki, Bwana. Tusaidie, usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu aje tena, amwagwe juu ya watu. Jalia Yeye aje sasa, Bwana. Jalia kila mtu aliye mgonjwa aponywe. Kila mwenye dhambi aokolewe, kila anayetafuta ajazwe. Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Mara moja tu zaidi, Bwana! Mara moja zaidi jalia Roho Mtakatifu ashuke miongoni mwa watu!

219 Inueni mioyo yenu sasa, na mlie, "Mara moja zaidi, Bwana!" Sote pamoja, "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" [Kusanyiko linashangilia na kulia kwa sauti kubwa, "Mara moja zaidi, Bwana!"—Mh.]

220 Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi jalia Roho Mtakatifu achukue wasikilizaji hawa, avunjilie mbali nguvu za adui, na kujaza kila mshipa na ubatizo wa Roho!

*Mara Moja Zaidi* SWA63-1117
(Once More)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 17 Novemba, 1963, katika Marc Ballroom huko New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org